ETIMOLOJIA YA MAJINA YA MAHALI YA KASKAZINI UNGUJA NA JINSI YANAVYOAKISI UTAMADUNI WA WATU WA KASKAZINI UNGUJA

SADA YUSUF ALI

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI YA (M.A KISWAHILI - ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo: **“Etimolojia ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Unguja na Jinsi Yanavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Kaskazini Unguja”** na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili (M.A.Kiswahili - Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…….

Dkt: Hanna Simpassa

(Msimamizi)

……..…….

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile ya Tasnifu hii kama kutoa sehemu ndogo ya tasnifu hii, kielektroniki au njia nyegine yoyote ile bila ya idhini ya Muandishi wa Tasnifu hii au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi, **Sada Yusuf Ali**, natamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii *Etimolojia ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Unguja na Jinsi Yanavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Kaskazini Unguja* ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa na wala kutohudhurishwa popote kwa lengo la kufuzu shahada kama hii.

……

Saini

……

Tarehe

TABARUKU

Napenda kutabaruku kazi hii kwa mume wangu mpenzi Bw. Massoud Sharif kwa msaada wake wa hali na mali kwani alikuwa pamoja na mimi kwa kila kitu katika utafiti huu. Pia napenda kumtabaruku mlezi wangu ambaye ni bibi yangu mpenzi Bi. Sada Ayoub kwa kunipa malezi bora. Pia nawatabaruku wazazi wangu Bi. Fatma Swaleh na Bw. Yusuf Ali kwa kunisomesha mpaka nikafikia hatua hii.

SHUKURANI

Natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Allah (S.W) ambaye ni mmiliki wa hii dunia na vilivyomo, kwa mapenzi yake amenipa uwezo na uzima kwa ajili ya kumtumikia yeye maamuzi yake yameniwezesha kufanya kazi hii ya utafiti. Nitakuwa mchoyo wa shukurani kama sijawashukuru wote walionisimamia na kuniongoza katika utafiti huu, miongoni mwao ni msimamizi wangu wa kazi hii ya utafiti kwa kunipa muongozo na kunifundisha kwa kina jinsi ya kufanya utafiti huu naye ni Dkt Hanna Simpasa. wa Chuo Kikuu huria cha Tanzania na wahadhiri wangu wengine kama vile mwalim Bakari Kombo, Dkt Omari Muhamedi kwa msaada wao ambao umeniwezesha kufanya kazi hii.

Pia napenda kuwashukuru walezi na wazazi wangu kwa msaada adhimu kwangu katika maisha yangu yote ya masomo kuanzia mwanzo hadi leo kwa juhudi zao za kunilea tangu utotoni hadi muda huu, kwa kweli wamenipa malezi bora katika maisha yangu kiasi cha kupigiwa mfano katika jamii. Kadhalika napenda kumshukuru mtima wangu wa moyo ambaye ni mume wangu kipenzi Bw. Massoud Sharif kwa msaada wake wa dhati katika kazi hii ameweza kushiriki kikamilifu, kwani amekuwa na mimi bega kwa bega kwa kunipa kila ninachokihitaji katika kazi hii, ikiwemo pesa za kununulia baadhi ya vifaa vinavyohitajika, pia amenisaidia mawazo katika kazi hii ya utafiti.

Pia sitaacha kumshukuru mlezi wa mtoto wangu ambaye ni mdogo wangu kipenzi Fatma Said kwa kunilelea mwanangu kwa dhati na nikapata muda mkubwa wa kushughulikia utafiti huu. Mwisho kabisa napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu

wote, wakiwemo marafiki zangu, na walimu wangu wote wa Chuo Kikuu huria cha Tanzania kwa kushirikiana nao katika kukamilisha utafiti huu.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja, lengo hili liligawiwa katika malengo mengine madogo madogo mawili ambayo ni Kueleza asili ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na Kujadili jinsi majina ya mahali ya kaskazini Unguja yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja. Matokeo ya utafiti huu yalikusanywa kwa njia ya hojaji, dodoso na majadiliano, ambapo watafitiwa wapatao 76 wakiwemo wazee 20, vijana 50 na wafanyakazi wa mambo ya kiutamaduni 6 wote hawa walitoa ushirikiano mkubwa katika upatikanaji wa taarifa muhimu ambazo mtafiti alikuwa anazihitaji kutoka kwao. Mtafiti aligundua kwamba majina ya mahali yana asili ambayo ina uhusiano mkubwa na jamii inayohusika, vile vile aligundua kwamba kuna majina ya mahali ambayo yanafanana na majina ya mimea, vyakula, wanyama na hata watu mashuhuri. Halkadhalika mtafiti aligundua kwamba kuna baadhi ya majina yana uhusiano wa moja kwa moja na utamaduni wa jamii husika. Hata hivyo kuna baadhi ya majina ya mahali ambayo yanabadilika kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, hivyo kwa watafiti wanaofuatia wanatakiwa wachunguze kwa kina etimolojia ya majina ya mahali yanavyoathiriwa na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **viii**

ORODHA YA MAJEDWALI ..... **xiv**

ORODHA YA VIAMBATANISHO ..... **xv**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI KWA UJUMLA **1**

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Mada 1

1.3 Tatizo la Utafiti 3

1.4 Tamko la Utafiti 6

1.5 Malengo ya Utafiti 7

1.5.1 Lengo Kuu 7

1.5.2 Malengo Mahsusi 7

1.6 Maswali ya Utafiti 7

1.7 Mipaka ya Utafiti 7

1.8 Umuhimu wa Utafiti 7

1.9 Vikwazo vya Utafiti 8

1.10 Mpango wa Utafiti 9

1.11 Hitimisho 9

SURA YA PILI 11

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA 11

2.1 Utangulizi wa Sura ya Pili 11

2.2 Mapitio Yanayohusu Utamaduni 11

2.3 Mapitio Kuhusiana na Majina 13

2.4 Mapitio Kuhusu Majina ya Mahali 19

2.5 Kiunzi cha Nadharia 22

2.5.1 Nadharia Jumuishi ya Giles 23

2.6 Pengo la Utafiti 24

2.7 Hitimisho 25

SURA YA TATU 26

MBINU ZA KUKUSANYIA DATA 26

3.1 Utangulizi wa Sura ya Tatu 26

3.2 Mkabala wa Utafiti 26

3.3 Eneo la Utafiti 26

3.4 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti 28

3.5 Mbinu za Kukusanyia Data 31

3.5.1 Mbinu ya Mahojiano 31

3.5.2 Mbinu ya Dodoso 33

3.5.3 Majadiliano 33

3.6 Njia ya Uchambuzi wa Data 34

3.7 Usanifu wa Utafiti 34

3.8 Hitimisho 35

SURA YA NNE 36

UCHAMBUZI WA DATA 36

4.1 Utangulizi 36

4.2 Kueleza Asili ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Unguja 36

4.2.1 Etimolojia ya Mtaa wa Nungwi 37

4.2.2 Etimolojia ya Mji wa Kidoti 38

4.2.3 Etimolojia ya Mtaa wa Kilimani 39

4.2.4 Etimolojia ya Mtaa wa Tazari 40

4.2.5 Etimolojia ya Mtaa wa Fukuchani 41

4.5.6 Etimolojia ya Kijiji cha Tumbatu 42

4.2.7 Etimolojia ya Kijiji cha Mkokotoni 42

4.2.8 Etimolojia ya Mtaa wa Muwanda 43

4.2.9 Etimolojia ya Mtaa wa Pale 43

4.2.10 Etimolojia ya Mtaa wa Mchangani 44

4.2.11 Etimolojia ya Mtaa wa Mkwajuni 44

4.2.12 Etimolojia ya Mtaa wa Moga 45

4.2.13 Etimolojia ya Mtaa wa Matemwe 46

4.2.14 Etimolojia ya Kijiji Gamba 46

4.2.15 Etimolojia ya Mtaa wa Chutama 47

4.2.16 Etimolojia ya Kijiji cha Kinyasini 47

4.2.17 Etimolojia ya Kijiji cha Kibeni 47

4.2.18 Etimolojia ya Kijiji cha Kivunge 48

4.2.19 Etimolojia ya Kijiji cha Pitanazako 49

4.2.20 Etimolojia ya Kijiji cha Muwange 49

4.2.21 Etimolojia ya Mtaa wa Bumbwini 50
4.2.22 Etimolojia ya Mtaa wa Misufini 51
4.2.23 Etimolojia ya Mtaa wa Makoba 51
4.2.24 Etimoojia ya Mtaa wa kidazini 52
4.2.25 Etimolojia ya Mtaa wa Mkungwa 52
4.2.26 Etimolojia ya Kijiji cha Jitenge 52
4.2.27 Etimolojia ya Kijiji cha Mangapwani 53
4.2.28 Etimolojia ya Mtaa wa Mtoni 53
4.2.29 Etimolojia ya Kijiji cha Mtambile 54
4.2.30 Etimolojia ya Mtaa wa Vijibweni 54
4.3 Majina ya Mahali Yanayofanana na Mimea au Miti 55
4.3.1 Etimolojia ya Jina la Mwembe Mweupe 55
4.3.2 Etimolojia ya Mzambarau Machoka 56
4.3.3 Etimolojia ya Kijiji cha Mwambale Mbalunguni 56
4.2.35 Etimolojia ya Kijiji cha Kinyasini 57
4.2.36 Etimolojia ya Mtaa wa Mafufuni 57
4.2.37 Etimolojia ya Jina la Mzambarau Mbata 57
4.2.38 Etimolojia ya Jina la Mdodo Pilau 58
4.2.39 Etimolojia ya Jina la Bumbwini 58
4.2.40 Etimolojia ya Jina la Mbuyu Popo 59
4.2.41 Etimolojia ya Jina la Kiembe Samaki 59
4.2.42 Etimolojia ya Jina la Paaguu 60
4.2.43 Etimolojia ya Jina la Khamisi Bweni 60
4.2.44 Etimolojia ya Jina la kwa Helefu 61

4.2.45 Etimolojia ya Mtaa wa Siti Mwinyi 61

4.2.46 Etimolojia ya Mtaa wa Makame Ng'ombe 61

4.3 Kujadili Jinsi majina ya Mahali ya Kaskazini Unguja Yanavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja 62

4.3.1 Mtaa wa Batini unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja 62

4.3.2 Mtaa wa Mdodo Pungwa' Unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja 63

4.3.3 Mtaa wa Muwange Unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja 63

4.3.4 Mtaa wa Mwembe Mgaa na Utamaduni wa Watu wa Unguja 64

4.3.5 Mtaa wa Mdodo Pilau Unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja 64

4.5.6 Kijiji cha Kivunge na Utamaduni wa Watu wa Unguja. 65

4.3.7 Mtaa wa Dunduwa na Utamaduni wa Watu wa Unguja 65

4.3.8 Mtaa wa Muwele na Utamaduni wa Watu wa Unguja 65

4.4 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti 66

4.5 Hitimisho 67

SURA YA TANO 68

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 68

5.1 Utangulizi wa Sura ya Tano 68

5.2 Muhtasari wa Utafiti 68

5.3 Hitimisho la Utafiti 70

5.3 Mapendekezo ya Jumla 70

5.4 Mapendekezo ya Tafiti za Baadae 71

MAREJELEO 72

VIAMBATANISHO 75

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Wilaya na Idadi ya Watafitiwa Wake 30

Jedwali Na. 3.2: Majimbo na Shehia Zake 30

ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatisho I: Maswali ya Dodoso kwa Vijana wa Mkoa wa Kaskazini Unguja 75

Kiambatisho II: Maswali ya Hojaji kwa Wazee na Wafanyakazi wa Mambo ya Kiutamaduni 78

Kiambatisho III: Maswali ya Majadiliano Kati ya Wazee na Vijana 80

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI KWA UJUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi ambayo imegawanywa katika sehemu kumi na moja. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa mada, sehemu ya pili inaelezea usuli wa mada, sehemu ya tatu inahusu tatizo la tafiti, sehemu ya nne inahusu tamko la utafiti sehemu ya tano inahusu mlengo ya utafiti. Sehemu ya sita maswali ya utafiti ambayo utafiti huu ulikusudia kuyajibu, sehemu ya saba inahusu mipaka ya utafiti, sehemu ya nane umuhimu wa utafiti, sehemu ya tisa vikwazo vya utafiti, sehemu ya kumi mpango wa utafiti na sehemu ya kumi na moja ni hitimisho.

1.2 Usuli wa Mada

Utafiti huu unahusu etimolojia ya majina ya mahali ya kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja. Unguja ni kisiwa kikubwa katika Bahari ya Hindi karibu na mwambao wa Afrika ya Mashariki mkabala na jiji la Dar es salaam. Pia ni kisiwa kikuu cha funguvisiwa vya Zanzibar ambavyo ni sehemu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Funguvisiwa ni kundi la visiwa vinavyokaa sehemu moja baharini, mara nyingi kundi hili lina asili ya pamoja kama vile kuwa mabaki ya kisiwa kikubwa zaidi kilichogawika kutokana na mmommonyoko wa ardhi au asili ya volkeno. Funguvisiwa kubwa kabisa duniani ni Indonesia pamoja na Ufilipino. Unguja ina eneo la takriban Km 1.658 ikiwa na wakaazi 460,000. Mji mkuu wa nchi yoyote ile ni mji ambao una maendeleo makubwa sana kwa kuwa ina miundo mbinu na huduma zilizo bora. Kwa mfano mji mkuu wa Tanzania ni Dar es salaam ingawa makao makuu ni Dodoma. Zanzibar ndiyo mji mkuu ambao uko kwenye

pwani ya Magharibi mkabala na Bara na una wakazi 206,292 kulingana na sensa ya mwaka (2002). Kisiwa cha Unguja kina mgawanyiko wa mikoa mitatu ambayo ni kati ya Mikoa 30 ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Mikoa hiyo mitatu ni Unguja Kaskazini, Unguja Kusini na Unguja Mjini Magharibi.

Watu wa Unguja ni Waswahili, ambapo Mswahili ni mtu mwenye asili ya mwambao wa Afrika ya Mashariki na ambaye lugha yake ya awali ni Kiswahili na kufuata utamaduni wake (BAKIZA, 2004). Pia Mswahili katika tasnifu hii tumelitumia kumaanisha mtu mwenye kiwango kikubwa cha umilisi wa lugha ya Kiswahili, na pia linamaanisha mtu ambaye amefungamana sana na mila na desturi, na jamii za watu watumiao lugha ya Kiswahili kiasi cha kumuathiri kifikra, kimtazamo, kiitikadi na kiimani (Ponera, 2013). Kiujumla tunasema kuwa Waswahili ni watu wa mwambao wa Afrika ya Mashariki ambao wanaongea lugha ya Kiswahili, wana tamaduni zao zinanazoendana na makabila yao, halkadhalika waswahili wamegawanyika katika makabila mbali mbali, baadhi yao ni Wapemba, Waunguja Wahehe, Wanyamwezi, Wadigo, Warangi, Wanyaturu, Wamakonde, Wandengereko na kadhalika.

Shughuli kubwa zinazofanywa na watu wa Unguja ni kilimo na uvuvi. Kama tujuavyo Kisiwa cha Unguja kimezungukwa na bahari, hivyo wakaazi wa visiwani mara nyingi hujishughulisha na uvuvi. Watu wa Unguja wanafanya shughuli za uvuvi kwa sababu ya kuwasaidia katika biashara, kwani uvuvi ni biashara ambayo ina kipato kikubwa. Wavuvi hawa wanakuwa wanatumia zana za kisasa kama vile maboti ya kisasa na nyavu. Zana hizi huwasaidia kupata samaki wengi sana kwa ajili ya kuuza na matumizi ya nyumbani.

Kwa upande wa kilimo ardhi ya Unguja ni mzuri sana kwa kuotesha mazao, hivyo watu wengi wa Unguja hujishughulisha na kilimo kwani hutumia vifaa vya kisasa kama vile matrekta amabayo huwarahisishia kazi za kilimo. Mazao wanayolima ni kama vile maembe, mananasi, machungwa, maembe, nazi, karafuu, mdalasini, pilipili na basibasi. Mazao haya huuzwa ndani na nje ya nchi Mazao yanayouzwa nje ya nchi ni karafuu basibasi mdalasini na pilipili.

Zanzibar ni muunganiko wa visiwa viwili ambavyo ni Unguja na Pemba kwa pamoja visiwa hivi vimezungukwa na bahari pande zote. Hali kadhalika, Zanzibar imekusanya mikoa mitano (5) ambayo miwili (2) iko upande wa Pemba ambayo ni mkoa wa Kaskazini Pemba na mkoa wa Kusini Pemba, na kwa upande wa Unguja ipo mikoa mitatu (3) ambayo ni Mkoa wa Mjini Magharib, Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mkoa wa Kusini. Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao mtafiti atashughulika nao una wilaya mbili ambazo ni: Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya Kaskazini B. Wilaya ya kaskazini A imekusanya majina ya mahali kama vile Mkokotoni,Mkwajuni, Nungwi, Kidoti, Gamba, Matemwe, Fukuchani, hivyo katika mkoa huu mtafiti ndio atashughulika nao katika kuchunguza majina ya mahali jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu waunguja.

1.3 Tatizo la Utafiti

Kwa kawaida kila kitu duniani kinakuwa na jina lake ambalo hutambulisha mtu, kitu, mahali, wanyama miti na mengineyo. Majina yamefasiliwa na wataalamu wengi miongoni mwao ni Mgullu (1999), Massamba na wenzake (2004), Kihore (2008), Khamiss (2011), Matinde (2012) na wengineo. Kwa mfano, Mgullu (1999) amesema majina ni maneno ambayo hutaja vitu, Matinde (2012) amesema jina ni neno ambalo

hutaja mtu, kitu, hali, dhana na tendo, kwa hiyo majina hutaja watu, vitu, mahali, vyeo, dhana na tendo, ambapo wote kwa pamoja wanaelezea dhana moja kwamba majina ni maneno ambayo hutaja kitu, hali, mahali dhana na tendo. Kwa mfano chungwa, wali, sahani, simu na mengineyo.

Mgawanyiko wa majina hutofautiana miongoni mwa wataalamu, kwa mujibu wa Mgullu (1999) anasema majina yapo ya aina sita ambazo ni majina ya pekee, majina ya kawaida, majina ya mguso, majina ya dhahania, majina -yanayohesabika na yasiyohesabika, na majina ya jamii. Habwe na Karanja (2004) wameeleza aina saba za majina nayo ni majina ya pekee, majina dhahania, majina ya jamii, majina ya kitenzi jina, majina yanayohesabika na majina ya mguso. Hali kadhalika Kihore (2009) ameainisha aina tatu za majina nayo ni majina mahsusi (pekee), majina jumuishi (kawaida) na majina ya kikundi (majina ya jamii), hivyo mgawanyo huu wa wataalamu umetofautiana kutoka mtaalamu mmoja hadi mwingine, lakini wataalamu wote hawa wamebainisha kundi la majina ya pekee ambapo majina haya hujumuisha majina ya watu, kwa mfano, Ali, Anna, Wahida Saidi, Fatuma nakadhalika; majina ya Miji kama, Nairobi, Dodoma; majina ya ya milima, mfano mlima Kilimanjaro, majina ya maziwa, Viktoria, Tanganyika; majina ya bahari kama vile-bahari ya Hindi na Atlantiki. Katika kundi la majina ya pekee ndio tunapata majina ya nayotaja mahali, ambapo kati ka majina haya ndio mtafiti ameamua kushughulika nayo.

Wanajamii hutoa majina ya mahali katika maeneo ya makazi yao kwa lengo maalumu. na malengo hayo huyajua wanajamii inayohusika. Majina ya mahali ni majina ambayo yanataja miji au mitaa katika maeneo ya mjini na vijijini. Kwa mfano, katika kisiwa cha Unguja tunapata majina ya mahali kama vile, Fuoni, Bububu, Muembe Tanga,

Kiembe Samaki, Magogoni, Magomeni, Kwerekwe, Migombani, Darajani, Mshelishelini, Kibweni na kadhalika.

Hivyo majina yote hayo yana asili zake ambazo hudokeza utamaduni wao. Kwa mfano, Haji, (2001) katika kazi ya uchanganuzi wa kiisimu jamii wa mfumo wa utoaji wa majina ya mitaa alichunguza asili ya mtaa wa kwa Mwinyi Mkuu kuwa asili yake ni jina linalotokana na mwinyi mkuu aitwae Muhammad bin Ahmad. Eneo hili ndipo alipojenga kasri yake na kufanya shughuli zake hadi leo ndiyo pakaitwa hivyo. Mtafiti ameitumia kazi hii kama moja ya marejeo ya kazi yake.

Msanjila na wenzake (2009:48) wanasema lugha ya mzungumzaji na utambulisho wake ni vitu ambavyo haviwezi kutenganishwa, hivyo uhusiano wa lugha na jamii ni mahusiano ambayo yamefungamana kwa pamoja katika jamii yoyote ile. Wameendelea kusema kuwa mchango wa lugha katika utambulisho huweza kuelezwa kwa njia mbali mbali ikiwemo uhusiano wa majina na familia, uhusiano wa majina ya vitu na uhusiano wa majina ya matukio muhimu katika jamii hivyo lugha ndio nguzo kuu ya kutambulisha jamii. Aidha majina ya mahali ni muhimu sana katika jamii kwani hutambulisha tamaduni za wanajamii hao.

Suala la majina ya mahali katika mkoa wa kaskazini Unguja ni jambo ambalo mtafiti ameona ni vyema kushughulika nalo kwani mitaa mingi ya kisiwa cha Unguja yamepewa majina kulingana na sehemu husika ilivyokuwa hapo awali na hii ni kwa sababu ya kudumisha utamaduni wao, na ndio maana pakapewa majina hayo ili watu waweze kufahamu tamaduni zao.

1.4 Tamko la Utafiti

Wataalamu wengi wamefanya utafiti unaohusiana na majina, wakiwemo wageni na wenyeji wa Tanzania. Kuna ambao wamefanya utafiti kuhusu majina ya kanga, majina ya mapango, majina ya utambulisho wa jamii, majina ya mahali na vijiji. Miongoni mwa wataalamu hao ni kama vile, Mlacha (1995) ametumia fasihi simulizi katika kuchunguza majina ya maeneo Pia Zubeir (2005) nae amechunguza asili ya majina ya mahali katika kisiwa cha pemba, Mzee (2014) katika utafiti wake ameonesha majina ya pepo za Makunduchi katika kuhifadhi utamaduni wa Makunduchi huku akielezea sababu za kupewa majina ya pepo za Makunduchi. Kwa mfano, mzimu wa maji pepo umeitwa hivyo kwa sababu maji baridi yaliyopo kwenye mzimu, pindi watu wakienda kwenye mzimu huo husema wanaenda maji peponi kutokana na ubaridi wa maji hayo.

Halkadhalika Zubeir (2015) katika kazi yake ya etimolojia ya majina ya mahali ya watu wa Pemba alichunguza asili ya jina la mtaa wa Mitiulaya na akaona kwamba asili ya jina hili ni kuwa Miti ulaya ni mmoja kati ya mitaa iliyopo katikati ya mji wa Wete ambapo katika utawala wa Wareno ndipo ilipopitishwa barabara kuu iliyounganisha mtaa huu na mitaa mingine ya mji wa Wete. Miti ya kivuli ambayo hutoa maua kila ufikapo mwezi wa Disemba iitwayo ***'Christmas tree'*** ilipandwa katika eneo hili. Miti hii mpaka leo hii ipo kwenye eneo hilo. Wakazi wa Wete wa wakati huo, waliamini kwamba miti hiyo ilitoka Ulaya, na wakaiita miti ulaya. Ingwa ametoa asili ya mtaa huu lakini hakuonesha unaakisi vipi utamaduni wa Wapemba.

Katika utafiti huu mtafiti alichunguza kwa kina etimolojia ya majina ya mahali ya mkoa wa Kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja

1.5 Malengo ya Utafiti

Malengo haya yamegawika katika makundi mawili lengo kuu na lengo mahususi

1.5.1 Lengo Kuu

Ni kuchunguza etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakaisi utamaduni wa watu wa Unguja.

1.5.2 Malengo Mahsusi

(i) Kueleza asili ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja

(ii) Kujadili jinsi majina ya mahali ya kaskazini Unguja yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja.

1.6 Maswali ya Utafiti

(i) Ni ipi asili ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja?

(ii) Je majina ya mahali ya Kaskazini Unguja yanaakisi vipi utamaduni wa watu wa Unguja?

1.7 Mipaka ya Utafiti

Mtafiti alichunguza majina ya mahali katika kueleza asili za majina ya mahali inayopatikana Mkoa wa Kaskazini Unguja.Hivyo mtafiti hakujihusisha hata kidogo majina ya aina nyengine kama vile majina ya watu, majina ya vyakula, majina ya familia nakadhalika. Halkadhalika hakutoka nje ya mkoa wa Kaskazini Unguja

1.8 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unalenga kusaidia katika nyanja mabali mbali, kwanza kutambulisha jamii yenyewe ya Mkoa wa Kaskazini Unguja kujua asili ya majina ya mahali na jinsi

yanavyoakisi utamaduni wao kwani kuna baadhi ya watu hasa vijana na watoto hawafahamu asili za majina ya mahali wanakoishi. Pia katika nyanja ya elimu itasaidia katika kutoa mchango mkubwa katika taaluma ya isimu katika suala zima la kukuza lugha kwani majina mengi ya mitaa hayajuulikani na wataalamu wa lugha hivyo itakua ni chanzo cha kupata misamiati mipya inayotokana na majina ya mahali. Vilevile matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wanajamii wote kuelewa historia ya taifa lao, kama vile matukio mbali mbali yaliyotokea na watu mashuhuri waliotoa mchango mkubwa katika kujenga jamii yao. Mintarafu ya hayo, utafiti huu utakuwa chachu kwa wanaisimu wajao kupata mwamko wa kuendelea kutafiti mambo yanayowakumbusha utamaduni wao. Mwisho, utafiti huu utawasaidia wanautamaduni kujua tamaduni tofauti tofauti zinazopatikana duniani.

1.9 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na vikwazo tofauti tofauti kama vile tatizo la muda. Utafiti huu ulitumia muda mkubwa kwani wakati mtafiti anafanya kazi yake ya utafiti, pia alikuwa na majukumu mengine kama vile masomo ya darasani katika kipindi hicho hicho cha kufanya utafiti wake, na vile vile alikuwa na majukumu mengine ya Kifamilia, hata hivyo mtafiti alitafuta muda wa ziada ambao ulikuwa ni wa mapumziko ili kuendelea na kazi yake.

Pia tatizo jengine sugu liliojitokeza katika utafiti huu lilikuwa upande wa watafiwa, kwani baadhi ya watafitiwa walikuwa wanatoa taarifa za uongo, hali hii aliibaini mtafiti kupitia kwa watafitiwa wengine, miongoni mwao walikuwa wanapoteza kumbukumbu hivyo mtafiti aliitumia jitihada ya ziada ili kuwafanya wakumbuke, kwani alikuwa anawakumbusha mambo ya zamani.

Tatizo jengine lilitokana na itikadi kwa watafitiwa kwani walikuwa wanaogopa kutoa taarifa. Baadhi ya asili ya mitaa ilitokana na mambo ya kichawi hivyo walikuwa na imani ya kuwa wenyewe wakijuwa kwamba wametoa siri zao wanaweza kukumbwa na matatizo, kutokana na hali hiyo mtafiti aliwatoa hofu kwa kuwahakikishia kwamba hakuna hata mmoja atakae andikwa jina lake katika utafiti huu.

Mwisho ni tatizo la mbinu ya mahojiano. Mbinu hii ilijumuisha wazee na vijana, Hivyo wakati wa mahojiano kulitokea kutokuelewana kati ya wazee na vijana, kuna baadhi ya wazee walipokuwa wanatoa taarifa vijana walipinga, wazee wakaona kwamba wanakosewa adabu na vijana wao, wakahamaki na kuondoka hali hii ikasababisha kutokupatikana kwa taarifa. Lakini mtafiti aliamua kutafuta siku nyengine kwa ajili ya mahojiano ya wazee tu.

1.10 Mpango wa Utafiti

Tasnifu hii inajumuisha sura kuu tano, Sura ya Kwanza inaelezea vipengele mbali mbali vya utangulizi wa jumla unaohusu mada hii. Sura ya Pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi, na kiunzi cha nadharia. Sura ya Tatu inazungumzia mbinu za utafiti; Sura ya Nne inahusu uwasilishwaji na uchambuzi wa data za utafiti, na Sura ya Tano inaelezea muhtasari wa matokeo ya utafiti, mapendekezo ya utafiti pamoja na hitimisho.

1.11 Hitimisho

Sura hii imebeba mwongozo wa sura zinazofuatia na imetoa picha kamili juu ya kile kilichofanyika ndani ya utafiti huu. Hivyo mwanzo wa Sura hii imezungumzia

utangulizi, pia tulielezea usuli wa mada, tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, mipaka ya utafiti, umuhimu wa utafiti na vikwazo vya utafiti na jinsi ya kuvitatua na hitimisho. Hivyo kumalizika kwa Sura hii ndio mwanzo mzuri wa sura ya pili ambayo inahusu mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA

2.1 Utangulizi wa Sura ya Pili

Sura hii inahusu maandiko ya wataalamu mbali mbali walioandika kuhusiana na mada hii. Ni dhahiri kuwa wanaisimu mbali mbali walishatafiti kuhusiana na majina, hivyo mtafiti alipitia kazi mbali mbali zinazohusiana na mada yake. Mtafiti aliangalia mapitio yanayohusu utamaduni, mapitio yanayohusu majina, na mapitio yanayohusu majina ya mahali, halikadhalika tutamaliza kwa kuelezea kiuzi cha nadharia.

2.2 Mapitio Yanayohusu Utamaduni

Jamii zote duniani zinakuwa na tamaduni zake, tamaduni ambazo zinatambulisha jamii hizo, kwa kuliona hilo mtafiti alipitia kazi tofauti tofauti zinazohusiana na mambo ya kiutamaduni, kama ifuatavyo:

Newmark (1988) anaeleza maana ya utamaduni kuwa ni mkusanyiko wa mila na desturi zote za jamii inayotumia lugha mahsusi kama njia yake ya mawasiliano. Ruhumbika (1978) anatofautiana na mawazo ya Newmark (kashatajwa) katika kueleza utamaduni kwa kupinga kwamba utamaduni wa binaadamu si mila na desturi zake na mambo yake tu bali utamaduni ni jumla ya juhudi zote za jamii fulani katika kila kipengele cha maisha katika umma, filosofia za maisha, mfumo wa sheria, mbinu za ulinzi na usalama wa nchi, taratibu za mgawanyo wa kazi za uzalishaji mali, mifumo ya ugawaji wa matunda ya kazi hizo na juhudi ya kuiwezesha jamii isonge mbele. Kwa maana hiyo utamaduni hujumuisha mambo yote ya muhimu ambayo yanafuatwa na kuendelezwa katika jamii fulani, kwani kila jamii inakuwa na tamaduni zake na zinatofautiana kati ya jamii na jamii nyingine.

Nao Krueber na Kluclchohn (1952) walikusanya zaidi ya maana 200 za utamaduni, kuna mitazamo miwili (2) yenye kiutatanishi yanayohusiana na utamaduni, kwanza “utamaduni ni yale mambo mazuri pekee yanayojengwa na jamii”, ilhali mtazamo mwingine unasema “utamaduni ni kitu kilicho kibaya kinachotokana na jamii fulani, kwa maana hiyo mambo mazuri yanatokana na mtazamo wa jamii husika wakati mambo mabaya yanatokana na mtazamo wa jamii nyingine, hivyo utamaduni hujihusisha na elimu inayohusu asili na maendeleo ya awali ya binaadamu pamoja na elimu ya ishara ambayo huelezea namna ya kujifunza kwa uvumbuzi, utamaduni, hutumika kuelezea mambo ya sherehe jando na unyago, matamasha mbali mbali, , ibada za wazi kama tambiko, hadithi tenzi na masimulizi mengine mabadiliko ya kiutamaduni, na yote hayo huwasilishwa kwenye televisheni na redio kupitia vipindi mbali mbali kama vile maigizo, vipindi vya sanaa na wasanii nakadhalika.

Sera ya utamaduni (1997) inaeleza maana ya utamaduni kuwa ni mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake, sera hii ina maanisha kuwa utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii mtazamo wa mambo na taratibu zao za maisha yao waliyojiwekea ambapo zinawatofautisha wao na jamii nyengine, utamaduni ndicho kielelezo muhimu cha uhai wa binaadamu hivyo umoja na mshikamano unatokana na utamaduni, vile vile nguzo kuu za kutambulisha utamaduni ni mila na desturi, sanaa na michezo na historia ya jamii.

Utamaduni wa Wazanzibari ni kwamba BAKIZA (2008) anabainisha kuwa “Mila za Wazanzibari ni juu ya yale waliyoyaamini kuwa yanawaletea upendo wa kuishi kijamaa, kimitaa au kivijiji. Mfano, kula kiukumbi, kuabudu pamoja na kusaidiana kiuvyawa au kiujima kwa malezi, uuguzi, ndoa, tiba wakati wa misiba, hivyo ni wazi

kwamba utamaduni wa Wazanzibari umejikita katika mila na desturi zao walizojiwekea, Wazanzibari wana mila ya kuoa mke mmoja hadi wanne.Pamoja na imani ya dini ya Kiislamu baadhi ya watu hawa wana mila za kufanyiana uchawi kwa lengo la kuhusudiana kwa kurogana, kupeana punju, mashetani, majini, kupelekeana chui, vizuu na kuwangiana…"

2.3 Mapitio Kuhusiana na Majina

Majina ni maneno ambayo huwakilisha kitu fulani, hali, au tendo, hivyo kwa kuwa mada yetu inahusu etimolojia ya majina, Mtafiti aliangaza kazi mbali mbali zinazohusiana na majina, miongoni mwao ni kama wafuatao.

Mgullu, (1999) ameeleza majina na aina zake kwa kusema kuwa kuna majina ya mhguso, majina ya kawaida, majina ya dhahania, majina yanayohesabika na majina yasiyohesabika, mtaalamu huyu amechanganya majina ya watu, mahali, milima, maziwa mito na bahari, na kuyaweka katika kundi moja la majina ya pekee, lakini ilikuwa ipo haja ya majina haya kubaguliwa na kuyaweka katika makundi tofauti kwani majina haya hayafanani kisifa, wala kitabia.

Funk (1997) akizungumzia suala la utoaji wa majina anasema utoaji wa majina ni tendo kama lilivyo tendo jingine na limo katika muktadha, pia masuala ya majina ya kupambanua na kuyatofautisha na jamii nyingine, hivyo anatueleza kwamba kila jamii inatoa majina kulingana na jamii yenyewe ilivyojiwekea. Hivyo ni dhahiri kwamba jamii moja haiwi sawa na jamii nyingine katika utoaji wa majina. Kwa mfano majina kama vile Asha Fatma, Ali Khamisi, Faki, Juma, Haji, Sada ni katika majina ya jamii ya Wazanzibari ambayo yanawatambulisha binaadamu.

Halikadhalika Massamba, na wenzake (2011) wametoa mchango mkubwa katika suala zima la lugha kupitia majina kwa kuelezea njia mbali mbali ikiwemo majina ya familia, uhusiano wa majina ya vitu, na uhusiano wa majina ya matokeo katika jamii, kwa mantiki hiyo ni wazi kuwa majina yamefungamana na mahusiano fulani katika jamii kwani jina hasa majina ya watu yanatokana na uhusiano; kwa mfano mahusiano ya kurithi, katika jamii yetu ya Wazanzibar watoto hupewa majina kwa kurithishwa jina la bibi yake au babu yake.

Omary (1970) alitafiti majina ya watu katika jamii ya *Chasu* na kueleza kuwa majina katika jamii ya Chasu yanatokana na vigezo kama muingiliano wa jamii za kigeni, hali ama sura ya nchi, pia matukio fulani. Ameeleza kuwa jina "Senkondo" hupewa mtoto wa kiume aliyezaliwa wakati wa vita na "Nankondo" hupewa mtoto kike aliyezaliwa wakati wa vita. Watoto wanaozaliwa katika kipindi cha jando/unyago wa kiume huitwa "Semshitu", na mtoto wa kike huitwa "Namshitu". Mtaalamu huyu aliweza kugundua kwa kina majina katika jamii ya Chasu na jinsi ambavyo mambo ambayo yalipelekea kuitwa majina hayo.

Braver (1979) alifanya utafiti wa namna ya utoaji wa majina katika jamii ya Wachina. Katika utafiti wake aligundua kuwa mtu mmoja katika jamii ya Wachina hupewa majina tofauti kulingana na nyakati tofauti ambazo anapitia katika maisha yake. Kwanza hupewa jina akiwa mtoto, akiwa shuleni, baada ya kuoa au kuolewa, hupewa jina kulingana na nafasi yake ya kazi. Naye Chulk (1992) alitafiti majina ya watu wa Nigeria ambapo alieleza kuwa kawaida watu hupewa majina kutokana na matukio fulani, au vitu vikubwa vya kushangaza ,au siku ama juma mtu aliozaliwa. Agyekum (2006) alifanya utafiti kuhusu majina ya watu wa kabila la Akan nchini Ghana na

aligundua kuwa watu wa kabila la Akan huwapa watoto majina kulingana na siku wanazozaliwa, majina yanayotokana na familia,majina wanapopatiwa tohara (jando), majina yanayotokana na athari za kimaumbile, majina ya watoto wanapozaliwa pacha (wawili ndani ya mimba moja), majina ya kidini, majina ya kimiujiza, majina yanayotokana na mafanikio, majina ya vijembe na methali (mafumbo), majina ya umbo la mwili wa mtoto aliyezaliwa na majina ya ukoo.

James (2011) alitafiti kuhusu maana za majina ya watu wa kabila la Lulogooli liliopo magharibi ya Kenya katika utafiti wake aligundua kuwa kuna makabala miwili ya kimaana katika majina ya watu wa kabila la Lulogooli.Mkabala wa kwanza ni mkabala wa maana halisi na mkabala wa pili ni mkabala wa maana kimatilaba. wataalamu wote hawa wameishia tu katika majina ya watu, lakini hawakueleza hata kidogo majina ya aina nyengine kama vile majina ya mahali, majina ya jamii, majina ya vitu nakadhalika.

Chulk (1992) alitafiti majina ya watu wa Nigeria ambapo alieleza kuwa kawaida watu hupewa majina kutokana na matukio fulani, au vitu vikubwa vya kushangaza, au siku, na juma mtu aliozaliwa. Mfano "Aiende" Kiyoruba lina maana ya tuliyekuwa tumemuomba/subiri. Jina hili limetokana na familia ambayo muda mrefu haijapata mtoto wa kiume.Utafiti huu umechunguza maana za majina hivyo umemsaidia kugundua kuwa katika majina kuna maana zinazojificha na hujulikana na jamii au familia yenyewe tu.

Muzale (1998) amefafanua kuwa kutoa jina ni kutoa maana, majina ya binaadamu yanaweza kutusaidia kuwa na mkabala mwingine katika isimujamii au isimu historia,

maelezo haya yanaonesha dhahiri kwamba utoaji wa majina una maana kubwa katika jamii miongoni mwa maana hizo ni kuitambulisha jamii husika kutokana na mila zao,desturi na utamaduni, kwa mfano jumba la makumbusho lililopo Zanzibar linaonesha mambo mengi ya makumbusho yakiwemo vyungu vya kupikia, mikoba ya ukili, makawa, masanamu, misalaba, gari alokuwa akitembelea Raisi wa kwanza wa Zanzibar Mheshmiwa Abeid Amani Karume. Mambo yote haya ni ya zamani na yanatokana na jamii ya Zanzibari ambayo ni katika kuendeleza utamaduni kwani hadi leo kuna baadhi ya watu wanatumia mikoba ya ukili katika safari zao hali kadhalika wanatumia vyungu kwa ajili ya kupikia.

Mutembei (2009) akimnukuu Haji (2014) anauliza kwanini watu huwapa watu majina, pahali,vitu, hali au matukio? Jee jina ni jina tu au lina maana yake? Jee ni utambulisho au kielelezo cha yale yaliyopita au utabiri wa yale yatakayotokea. Akijibu maswali hayo Mutembei (kashatajwa) anaeleza kuwa “kwa vyovyote vile huwa kuna msukumo fulani unaofanya watu watoe majina, ama kwa hakika majina tunayopewa mara nyingi huwa na utambulisho na asili zetu, baadhi ya majina yanamtambulisha mtu, eneo analotoka, sifa na tabia, majina ni sehemu mzuri ya kila utamaduni, majina yana umuhimu mkubwa kwa watu wote, watu hupewa majina kutokana na jamii wanayotoka, kupitia majina mtu hujuahistoria ya jamii,pia majina hutofautisha matendo ya mtu mmoja na mwingine, uhusiano wa majina na utambulisho ni aina ya alama na mahusiano kati ya mtu na jamii, kwa kumpa mtu jina jamii inatambua uwepo wake, kwa hivyo mtafiti aliona ipo haja ya kuelezea asili ya majina katika jamii ili jamii hiyo iweze kujitambua yenyewe halkadhalika na kutambuliwa na watu wengine.

Seif, (2011) anasema majina ya watu hupewa watoto kutokana na matukio mbali mbali, kama vile njaa, ugomvi, vita, kufa kwa watoto wanapozaliwa na kufuata koo zao. Kwa mfano Jongo. Panzi, Mtama, Mwinyijuma, Mwinyijongo nakadhalika, majina haya yote ni katika majina ya jamii fulani ambayo yanatokana na sababu za njaa, vita matukio mbali mbali na kadhalika.

Msanjila na wenzake (2009) walitafiti majina ya matukio yaliyoikumba jamii ya Wagogo ambayo yamepewa majina kwa lugha ya Kigogo, waliwapa majina hayo ili kuwa sehemu ya utambulisho wao kwa mfano jina la ‘Magubika’ jina hili lilitokea miaka 1988 na 1989 lililofanya watu wafunike vyungu vya kupikia kwasababu kulikuwa hakuna chungu hata kimoja cha kufunikia, ‘Hambaya’ jina hili lilitokana na jamii ya Wagogo ambalo watu walikuwa wakila chakula lakini hawashibi, njaa hiyo ilitokea miaka ya 1949, kwa kiasi fulni mtaalamu huyu alifanikiwa kuyaonesha majina yanayowatambulisha wagogo kutokana na matukio mbali mbali lakini alikuwa aeleze japo kidogo majina ambayo yanaonesha utamaduni wa Wagogo.

Pia Masanjila na wenzake wameshatajwa walitaja majina ya Kiswahili ambayo hutambulisha Tanzania na Afrika yao majina waliyoyataja ni kama vile Mlima Kilimanjaro, chakula aina ya ugali, mnyama twiga, ziwa Tanganyika, kwa vile Tanzania ni nchi tajiri kwa mambo ya utamaduni mtaalamu huyu ameacha pengo kubwa kwa kuwa hajaelezea hata kidogo utamaduni wa Tanzania hivyo kwa watafiti wanaokuja wanapaswa waliangalie suala hili na kulichunguza kiundani zaidi.

Mwansoko akinukuliwa na Haji, (2014) katika ripoti yake ya utafiti iliyofanyika viwanda mbali mbali, katika ripoti yake ya mji wa Tanga na Dar es salaam kuhusu

majina ya biashara ya Kiswahili, anaeleza kuwa uzalishaji wa bidhaa viwandani ulitokana na uibukaji wa majina ya kibiashara mengi yao yakiwa katika lugha ya Kiswahili, wenye viwanda walilazimika kubuni majina ya biashara, hivyo walitumia njia mbali mbali zilizotumika katika kubuni majina hayo kama vile walitumia njia ya sitiari na wakapata majina mengi, mfano wa majina hayo ni 'simenti chapa simba', 'sabuni chapa kiboko', pia walitoa majina ya lugha nyingine, ili kupata majina ya biashara kwa mfano neno 'form' lenye asili ya Kingereza walilichukua na kuliita foma na kulitumia katika biashara zao, pia walitumia majina ya kijografia kama vile 'Ambon plastiki', 'mlima Kilimanjaro', hivyo mtaalamu huyu alijua uwepo wa majina haya na ndipo akaamua kuyafanyia uchunguzi, na imewasaidia wanajamii wengi kujua majina hayo ya kibiashara.

Pandu, (2014) katika utafiti wake wa majina ya shule za Unguja mjini katika kutunza historia ya Wazanzibari ametaja shule mbali mbali, zikiwemo Benbella, Haelesali, Darajani, Vikokotoni, Muembeshari, Muembemakumbi, Bububu, Kwerekwe, nakadhalika, pia katika utafiti wake ameeleza historia ya Zanzibar kuwa ni Persion' au Waarabu wa Persion wamelitoa jina hili kutoka katika neno Zenji Bar lenye maana ya Negro cost Waarabu wamelitoa jina hili kutokana na Zayns al bar lenye maana ya nchi yenye usawa au neema ya nchi hiyo.

Utafiti mwingine ni ule uliofanywa na Rubanza (2001) kuhusu ubunifu wa kiisimu wa majina ya watu katika lugha ya Kihaya, lengo kuu lilikuwa ni kuonesha ubunifu wa jamii hiyo na jamii nyingine ambayo ilihusisha na jamii ya Wayoruba, utafiti wake ulijikita zaidi katika uchambuzi wa kimofolojia unaohusika katika majina ya mahali, akiendelea kufafanua Rubanza (kashatajwa) anasema majina huwakilisha viwango

vitatu, kiwango cha kileksika, kiwango cha kuhusisha na kiwango cha onomostiki, mtaalamu huyo ameeleza kuwa majina ya Kihaya huwa yana maana inayozingatia mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto anayepewa jina hilo, hali ya kipato cha familia, mfuatano wa watoto katika kuzaliwa na migongano ya kijamii, hivyo mtaalamu huyu amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuonesha ubunifu wa hali ya juu wa kulinganisha majina ya jamii moja na nyingine

2.4 Mapitio Kuhusu Majina ya Mahali

Katika kazi zilizopitiwa hapa ni zile zinazohusu majina ya mahali na maana zake pamoja na kazi zilizoeleza vigezo vilivyotumika kutolea majina ya mahali na matukio yaliyosababisha kuitwa majina hayo, miongoni mwa kazi hizo ni kama zifuatazo;

Haji (2014) akimnukuu Lyon akielezea neno maana kuwa ni dhana au wazo inayosafiri kutoka katika akili ya msomaji hadi kufikia katika akili ya msikilizaji, hivyo ni dhahiri kwamba kila kitu duniani kinakuwa na ufafanuzi wake na ndio maana tukapata maana ya kila kitu, kitu chochote kile huwa hakiitwi hivyo isipokuwa kuna jambo fulani lililoisukuma kitu hicho kuitwa hivyo, na ndio maana mtafiti akaamua kuchunguza majina ya mahali kwa kueleza asili yake au historia ya kuitwa kwa majina hayo.

Pia Haji (kashatajwa) katika utafiti wake ameeleza majina ya mahali huitwa kulingana na matukio fulani kwa mfano jina la Mwananyamala limeitwa hivi kwa sababu jina hili limepatikana katika Mkoa wa Dar es salaam likiwa na maana ya kuwa kulikuwa na mtu ambaye alikuwa na watoto wawili, watoto hao walitumbukia katika shimo, mmoja akazama na kupotea, lakini watu walikuwa wanamsikia akilia na

chunusi anambembeleza ‘nyamala mwanangu’ nyamala mwanangu’ likiwa na maana mtoto usilie na ndio maana pakaitwa Mwananyamala.

Cameroon (1961) anaeleza utoaji wa majina ya mahali katika jamii ya Waingereza. Ametoa aina mbili. Kwanza ni yale yanayohusiana na makaazi, kwa mfano Stanford Bridge ni sehemu yenye daraja. Pili ni yale yanayohusiana na sura ya nchi ya eneo hilo. Mfano “Greenhill” ikimaanisha eneo lenye kilima chenye kijani kwa wingi. Hymen (1964) anaeleza majina ya mahali yanaakisi fikra, watu, pia vipengele vya utamaduni. Rey (1995) anaeleza majina yanayotumika kutambulisha watu au mahali yanaonesha utofauti baina ya jamii moja na nyingine, kutokana na vigezo vya asili, historia na utamaduni.

Schotsman (2003) anaeleza historia ya maana ya mahali katika jiji la Dar es salaam, alitumia majina ya vituo vya daladala na majina ya mitaa /kata. Alieleza majina ya vituo vya mabasi yanatokana na majengo kama shule hospitali, kanisa, watu maarufu, shughuli zinazofanywa na watu katika eneo hilo. Pia mwelekeo wa kituo kilipo kwa mfano, njia panda kwa Kawawa. Kituo hiki kipo njia inayoelekea kwa Kawawa. Pia anaeleza majina ya mitaa yanatokana na mimea iliyopo katika sehemu hiyo, lugha za asili mfano “Mwananyamala” maana yake ni ‘mtoto usilie’, Majina mengine hutolewa hutokana na maeneo ambayo yanashabihiana mfano ‘Mawenzi’ ya Dar es salaam ni eneo lenye mteremko kama mteremko ulioko ‘**Mawenzi**’ ya Kilimnjaro.

Massoud, (2014) kuhusu tafiti yake aliyofanya kuhusiana na mchango wa mjina ya vijiji vya Donge katika kuhifadhi historia ya Unguja kama vile Kipanga, Pangamena,Vijiweni, Chechela, Mapapai, Ndagoni, Mkarafuu, Pakacha, Chokwe

nakadhalika, katika vijiji vyote hivi alivieleze asili yake kwa kila kijiji, kwa mfano kijiji cha Bumbwi alisema kuwa kijiji hichi asili yake ni mtaa ambao hawaishi watu isipokuwa watu wanaokwenda kulima uwele na mtama, baadhi ya wakati wanapata mavuno mengi baadhi ya wakati wanapata mavuno machache, wakiwa wanaulizana umepata mavuno kiasi gani, mmoja wao akajibu nimepata mmoja tu wabumbwini na ndio maana pakaitwa bumbwini, mtafiti huyu amefanikiwa kwa kiasi fulani kueleza asili ya majina ya mitaa, lakini hakuangalia asili hiyo inaakisi utamaduni.

Juma, katika utafiti wake ameeleza majina ya mahali ya Bwejuu, Mtendeni Makunduchi na Kizimkazi kwa mfano alieleza asili ya mtaa wa Makunduchi kuwa asili yake ni kwamba inasemekana kulikuwa na kundi moja la watu lililokuwa kae huko pwani Unguja ukuu, baadhi yao wao waliondoka na kueleke kusini Mashariki ya hiki kisiwa kupitia sehemu mbali mbali hatimae wakafika hii sehemu yenye udongo mwekundu, hapo kundi hilo lilisita kwanza na kuanza shughuli zao za kilimo, baada ya muda fulani kulikuwa na kundi jingine likirudi kule pwani na walipokuwa wakiulizwa na wenzao hujibu”tuwa huko nyekunduchi” yaani wanaishi mahali ambapo ardhi yake ni nyekundu kwa kuwa hawakuweza kulipata jina hasa la mahali penyewe, hivyo tamko nyekundu liliwakalia wepesi zaidi, basi katika kulikariri neno hili, mara kwa mara wenyeji walifanya nyongeza ya herufi kidogo kidogo na ndimi nyingine zikianza tamko la makunduchi na kubaki hivyo hivyo hadi leo.

Chum (1982) anaeleza asili ya mitaa inayopatikana Mkoa wa Kusini Unguja. Anatoa mfano wa *Paje,* kwamba asili yake ni mnyama aitwae paa, pamoja na kilimo cha choroko. Miongoni mwa wageni waliofika Unguja walikuwa ni ndugu saba ambao walishauriana kuishi pembezoni mwa pwani ya Unguja ili waendeleze kilimo cha

choroko.Wakati wakijadiliana mmoja aliuliza, ‘tukiwa na kilimo hiki paa je? kwa vile paa wanapenda choroko tutaweza kukabiliana nao wasituharibie vipando vyetu?’.Ndio maana mahali hapo pakaitwa Paje.

Mlacha (1995) anaeleza asili ya mitaa inayopatikana kisiwani Pemba.*Uvuani,* asili yake walihamia wageni wakawa wanafanya shughuli za uvuvi, wakaja watu wakawauliza Uvuani, yaani unavua nini? Hapo ndipo kijiji hicho kikaitwa Uvuani. kwa upande wa neno *Micheweni,* walikuwepo watu wakatili wenye tabia ya kuwaua watu. Hivyo watu walioishi mbali na eneo hilo walipaita michawini linatokana na Uchawini lenye maana ya kuuwa, baadaye pakaitwa Micheweni.

Msanjila na wenzake(2009) walitaja majina ya Kiswahili ambayo huitambulisha Tanzania Afrika ambapo lugha ya Kiswahili inatambulika kuwa ni lugha ya Afrika hivyo alitumia majina ya mahali kama vile mlima Kilimanjaro, chakula aina ya Ugali, Ziwa Tanganyika, Twiga, majina haya yote yanapatikana Tanganyika, Twiga, ambayo ni majina maarufu sana Tanzania na wanaishi watu wa makabila tofauti tofauti. Roden amesema kuwa majina ya mahali yana maana na akaongezea kusema kwamba yanawakilisha utambulisho wa mtu mmoja mmoja uhusiano wa kifamilia wa hadhi na kazi inayofanywa,

2.5 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia imefesiliwa na wataalamu mbalimbali na kwa namna tofauti tofauti miongoni mwa wataalamu hao ni kama wafuatao. Sengo (2009:1) anafasili nadharia kuwa ni wazo kuu, fikra kuu mwongozo mkuu wa mtu, watu, au jamii, ya pahali fulani, wakati fulani na kwa sababu fulani.Nadharia ni mawazo, maelezo au

mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, (2013:414), nae Hudson (1985) anasema kuwa nadharia ni mahitimisho yanayotokana na uchambuzi wa data ambazo hujaribiwa, na ubora wake ukithibitika hutumiwa kama mwongozo wa utafiti. Kwa mantiki hiyo nadharia hubeba mawazo, dhana au maelezo yatolewayo kwa nia au kwa lengo la kueleza hali fulani chanzo au muundo wa jambo fulani, hivyo nadharia ni dira la kulikubali jambo kiimani, kifalsafa, kidini na kiutamaduni, nadharia huundwa kwa kutumia data za kitakwimu na data za kimaelezo katika kulichambua jambo linalohusika.

2.5.1 Nadharia Jumuishi ya Giles

Hii ni nadharia ambayo mtafiti aliitumia katika kazi yake, kutokana na kuwa nadharia hii imefungamana sana na jamii. Giles (1979) anafafanua kwamba utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamii lugha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii. Majina ni moja wapo kati ya mambo yanayobaisha jamii, hivyo nadharia hii ni yenye kufaa katika kutafiti asili za majina ya mahali jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja.

Msingi wa nadharia hii jumuishi unazingatia fasili ya jamiilugha inayosema “jamii inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamiilugha moja ambayo iko tofauti na jamii lugha nyingine” (Giles, 1979:253). Fasili hii ya jamii lugha, mbali na kuwa msingi wa nadharia hii jumuishi pia ni msingi wa maana halisi ya utambulisho.

Maana halisi ya utambulisho kwanza ni kuwa jamiilugha yenyewe hujitambua kuwa iko tofauti na jamiilugha nyingine katika masuala msingi kama utamaduni, mila na

desturi, imani (dini) chakula, mavazi, uchumi au siasa, kwa kweli nadharia hii ya Giles inaonesha uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii, pia inaonesha nguvu za lugha jinsi zinavyotumiwa na wataalamu au wanajamii kuweza kubainisha utambulisho wa jamii husika.

Watafiti waliowahi kuitumia nadharia hii ni pamoja na Haji, (2001) ambaye alitumia nadharia hii kuchunguza maana ya majina ya watu wa jamii ya Pemba, Hali kadhalika Zubeir (2005) aliitumia nadharia hii kwa kuchunguza asili ya majina ya mahali ya watu wa Pemba. Hivyo kupitia nadharia hii iliwasaidia sana katika kazi zao kwani walichunguza majina kwa kuhusianisha na jamiilugha. Kwa kuwa majina ya mahali huweza kuaathiriwa na jamii fulani katika utoaji wa majina hayo, hivyo mtafiti alipendelea zaidi kuitumia nadharia hii kutokana na sababu zifutazo.

Kwanza, mtafiti iliweza kumsaidia wakati wa ukusanyaji wa data jinsi ya kuelezea majina ya mahali na kwa vipi yanawatambulisha wanajamii husika. Pia wakati wa uchambuzi wa data Mtafiti alipochambua data alifanikiwa kukamilisha lengo lake kwani alibaini kwamba wanajamii wa Unguja walikuwa na mambo ambayo yanaitambulisha jamii hiyo.

2.6 Pengo la Utafiti

Kwenye sehemu hii, mtafiti alisoma kazi tangulizi na akagundua kwamba dhana ya majina ni dhana pana sana, kwani wataalamu wameielezea kwa namna tofautitofauti,kuna walioelezea majina ya watu, majina ya familia, majina ya mitaa, majina ya pepo nakadhalika. Ni dhahiri kwamba sehemu yoyote ile hupewa jina kutokana na watu mashuhuri, shughuli fulani au historia fulani ya sehemu hiyo.hivyo

wataalamu wote hao wameacha pengo ambalo linahitajika kushughulikiwa, hivyo mtafiti akaona ipo haja ya kuchunguza majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja, hivyo mapitio yote hayo yalimsaidia sana mtafiti kwani kupitia kazi hizo ndizo zilikazomuongoza katika kufanya kazi yake kiufundi na kiufasaha.

2.7 Hitimisho

Sura hii ilikuwa ni sura inayozungumzia mapitio mbali mbali ya kazi tangulizi zinazohusiana na mada yetu, tuliangalia mapitio yaliyohusiana na tamaduni, mapitio yaliyohusiana na majina pamoja na mapitio ya majina ya mahali, kiuzi cha nadharia ambapo tumeelezea nadharia jumuishi ya Giles, tumemalizia na pengo la utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA KUKUSANYIA DATA

3.1 Utangulizi wa Sura ya Tatu

Katika Sura hii tutaeleza mbinu zilizotumika katika kukusanya data. Hivyo sehemu hii tutaigawa katika sehemu nyingine ndogo ndogo ambazo ni mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya utafiti, jinsi ya kuchaguwa watafitiwa wako (usampulishaji) mbinu zilizotumika kukusanyia data, njia zitakazotumika kuchambulia data, na kuhalalisha usanifu wa utafiti.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia mkabala wa maelezo na wa kitakwimu ambao unahusisha ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa moja kwa moja kwa njia ya dodoso, mahojiano na hojaji. Hivyo mtafiti ameyakusanya maelezo ya watafitiwa na kuyaweka katika asilimia za watu waliojibu, kwani inakuwa ni rahisi kwa mtafiti kupata data zake kwa wepesi. Mkabala wa maelezo ulitumiwa na mtafiti kwa kukusanya mawazo na hoja za watafitiwa kwa ajili ya kuzichanganua.

3.3 Eneo la Utafiti

Kwa kuwa lengo la utafiti huu ni kuchunguza etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja hivyo watu wa jamii ya Unguja imekusanya sehemu mbali mbali na sehemu hizo zimegawanywa katika Mikoa mikuu mitatu, ambayo ni Mkoa wa mjini Magharib, Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini, mtafiti ameamua kuchagua eneo la Mkoa wa Kaskazini Unguja ambapo Mkoa wa Kaskazini Unguja ni mmoja kati ya mikoa 30 ya Tanzania

umejumuisha Wilaya mbili (2) Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B, ambapo una wakaazi wapatao 136,953, wilaya ya kaskazini A ina wakaazi wapatao 84,348 kwa upande ya wilaya ya kaskazini B kuna wakazi wapatao 52,605 ambapo Wilaya hizi zote kwa pamoja zimekusanya mitaa kama vile Mkokotoni, Mkwajuni, Mahonda, Fukuchani, Nitope, Nungwi, Donge, Fumba,Matemwe, Pwani Mchangani, Kiwengwa, Kirombero, Tumbatu,Jongowe Muwanda, Kinyasini Moga, Shindoni, Kilimani, Tazari,Bumbwini, Mangapwani, Gamba nakadhalika.

Mtafiti ameamua kuchagua mkoa wa Kaskazini Unguja kwa sababu kuna mchanganyiko wa watu tofauti tofauti, na watu hao wanajishughulisha na shughuli mbali mbali kama vile uvuvi, kilimo, ufugaji, na biashara ambazo hizi ni shughuli zao kubwa wanazozifanya, shuguli ya kilimo inahusisha mazao tofauti tofauti, kama vile, maembe, machungwa, mihogo, viazi, tungule, mpunga, nazi na mengineyo, ambapo katika kilimo hicho wanatumia zana za kisasa kama vle trekta, pia wanatumia zana za kizamani, kama vile majembe,jambia mapanga nakadhalika, mazao haya ni kwa ajili ya matumizi yao ya nyumbani kwao na kwa ajili ya biashara, katika shughuli ya ufugaji wakaazi hawa hujishughulisha na ufugaji wa mbuzi, ngombe, kuku, bata, na wengineo wanyama hawa hupatiwa malisho mengi ili waweze kunawiri, hivyo huwasaidia kupata faida kubwa pindipo wanapowauza, katika shughuli ya biashara hujishugulisha na biashara mbali mbali kama vile mazao, nguo, mikoba nakadhalika katika biashara zao hizi husafiri sehemu mbali mbali kama vile Dubay kwa ajili ya kupata mavazi kama vile mabuibui, nguo, mitandio,mikoba, viambaa, hivyo huwasaidia wao kupata faida kubwa kuliko wakibakia katika mkoa wao tu, na pia hutumia uvuvi wa kisasa kama vile maboti ya kisasa nyavu, mabomu, mishipi,

mademe, ndoana, vidau na vyenginevyo, ili wapate urahisi wa kuvua samaki wengi. Mintarafu ya hayo Mkoa huu wa Kaskazini una mambo mengi ya asili na yenye historia, ya utamaduni wao, pia kuna mambo mengi ya kijadi yanayoheshimika kama vile, mzimu, ngoma za pungwa, mihanga nakadhalika, mambo ambayo yanaendelezwa kutoka kizazi hadi kizazi, hivyo mtafiti ameamua kufanya utafiti katika eneo hili kwa sababu majina yake ya mahali yana historia ya utamaduni wao.

Mitaa ambayo mtafiti alishughulika nayo ni Nungwi, Kidoti, Kilimani Tazari, Fukuchani, Tumbatu, Mkokotoni, Muwanda, Pale, Mchangani, Mkwajuni, Moga Matemwe, Gamba Chutama, Kinyasini, Kibeni, Kivunge, Pita na zako, Muwange, Bumbwini, Misufini, Makoba, Kidazini Mkungwa, Jitenge, Mangapwani, Mtoni, Mtambile, Vijibweni, Mwembe mweupe, Mwembe machoka, Mwambale mbalungini, Kinyasini, Mafufuni, Mzambarau mbata, Mdodo Pilau, Mbuyu popo, Kiembe samaki, Paaguu, Khamisi bweni, Kwa Helefu, Siti Mwinyi, Makame Ng'ombe, Batini, Muwembe mgaa, Dunduwa na Muwele.

Mtafiti amechagua mitaa yote hii kwa sababu ndio mitaa ambayo ni mashuhuri kwani inafahamika sana na wenyeji, na pia ni mitaa ambayo ipo kwa ajili ya kuitambulisha Unguja. Halkadhalika ni mitaa ambayo ipo karibu na mtafiti hivyo inakuwa ni rahisi kwake kupata data.

3.4 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti

Sampuli ni watafitiwa ambao wameteuliwa kutoka katika kundi kubwa ili watumike katika utafiti (Kothari, 2004, Enon, 1998, Best na Kahn 1993), Sampuli ni seti ndogo ya kundi lengwa ambayo mtafiti ataitumia kukusanya taarifa za utafiti wake (Julius

Caeser 1998). Hivyo watafitiwa hawa wanaweza kuwa watu, wa wanyama, vitu, miti nakadhalika ambapo mtafiti atatumia watafitiwa wachache ili kuwakilisha wengine, mtafiti aliteua sampuli ya wazee 26 na vijana 30 katika utafiti huu ameteua sampuli hii kwa sababu wazee ndio wenye ufahamu wa kutosha kuhusiana na nasili ya mitaa yao, vile vile vijana nao wansimuliwa asili za mitaa kutoka kwa wazee wao kwa upande wa usampulishaji, wataalamu wengi wamefasili dhana hii, miongoni mwao ni:

Kothari (2004) yeye anasema usampulishaji ni ile hali ya kuchagua mbinu mbali mbali za uteuzi wa washiriki au wahojiwa katika kundi kubwa la watafitiwa ili kuwapa majumuisho ya jumla, Kumar (1999) usampulishaji ni ile hali ya kuchagua idadi ya watu kwa ajili maswali katika utafiti. Hivyo usampulishaji ni namna ya kupata sampuli, kwa maana kwamba ule mfumo mzima wa kuchagua vitu, watu wachache ambao ni lengwa kutokana na kundi kubwa la watafitiwa kwa ajili ya utafiti ili kuwakilisha watu wengine, mtafiti atateua aina mbili za usampulishaji, kwanza aliteua sampuli nasibu inayopatikana kwa bahati ambapo kila mtafitiwa ana nafasi sawa ya kuteuliwa kama sampuli ya watafitiwa hapa mtafiti aliteua wazee 20 wowote wale wanaoishi mkoa wa kaskazini Unguja wakiwemo wanawake nane (8) na wanaume kumi na mbili (12), vilele mtafiti aliteua vijana 50 wa mkoa wa kaskazini Unguja wakiwemo wanawake ishirini (20) na wanaume thelethini (30), pia mtafiti aliteua sampuli tabakilishi ambayo mtafiti aliteua watafitiwa wake kulingana na matabaka yaliyomo katika jamii, mtafiti aliteua tabaka la kielimu kwani aliwateua wale ambao wamesomea mambo ya kiutamaduni ambao ni wafanyakazi na wenye dhamana ambao ni wasemaji kuhusiana na mambo ya kiutamaduni, watanyakazi sita (6) waliteuliwa kulingana na nafasi zao za kazi, na idadi yote hii ya watafitiwa

itagawiwa kwa mujibu wa wilaya ya Kaskazini A na wilaya ya Kaskazini B, na itaoneshwa kwenye jadwali lifuatalo.

Jedwali Na. 3.1: Wilaya na Idadi ya Watafitiwa Wake

	Wafanyakazi	**Wazee**	**Vijana**
Wilaya ya Kaskazini A	3	12	20
Wilaya ya Kaskazini B	3	8	30
Jumla	**6**	**20**	**50**

Chanzo mtafiti (2017)

Halikadhalika mtafiti aliteua aina ya usampulishaji lengwa ambayo ni aina ya usampulishaji ambayo huteuliwa na mtafiti kwa maksudi mazima, hapa mtafiti ametumi aina hii ya usampulishaji kwa sababu ya kupata data za uhakika, hivyo aliamua kuteua majimbo sita ya Mkoa wa Kaskaini ambapo kila Jimbo aliteua shehia zake, hii ni kutokana na kuwa ndio mitaa maarufu ambayo inajuulikana kila sehemu, na hii inajumuishwa katika jadweli lifuatalo:

Jedwali Na. 3.2: Majimbo na Shehia Zake

NA	**Jimbo**	**Shehia**
1	Nungwi	Nungwi, Tazari, Kilimani, Kidoti, Kilindi, fukuchani,
2	Mkwajuni	Mkwajuni, Matemwe, Gamba, Chutama, Kibeni, Moga,
3	Donge	Kimbiji, Mtambile, Mtoni, Kipange, Vijibweni,,
4	Bumbwini	Bumbwini, Makoba, Misufini, Kidazini, Mangapwani
5	Tumbatu	Tumbtu, Mkokotoni, Muwanda, Pale, Mchangani
6	Kijini	Kijini, Potoa, Kivunge, Kigongoni, Muwange, Pita na zako.

Chanzo mtafiti (2017)

3.5 Mbinu za Kukusanyia Data

Mbinu za ukusanyaji data ni njia na zana zitumikazo katika kukusanya taarifa za kiutafiti katika kutolea majumuisho. Kwa mujibu wa Kothari (2014) amesema mbinu ya kukusanyia data ni njia mbali mbali ambazo mtafiti anazitumia ili kupata data anazozihitaji katika utafiti wake. Kwa mujibu wa Panneerselvam (2012), data zimegawika katika makundi mawili ambapo anaona kuwa kuna data za msingi na data za upili. Panneerselvam (ameshatajwa) anaeleza kuwa data za msingi ni zile ambazo hukusanywa na mtafiti uwandani.

Data hizi kwa kawaida hukusanywa kwa matumizi ya sasa na baadaye, anaendelea kusema data za upili ni zile ambazo hukusanywa kutoka katika majarida, magazeti, machapisho na ripoti mbali mbali.kwa ujumla tunasema kwamba, Mbinu za kukusanyia data ni taratibu mbali mbali zinazotumika katika upataji wa taarifa kutegemea na malengo ya mtafiti aliyoyaweka., ili kuikamilsha shughuli ya ukusanyaji wa data ni muhimu mtafiti ateue mbinu mbali mbali anazoweza kuzitumia, katika utafiti huu wa etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja utajumuisha mbinu tatu ambazo ni hojaji mahojiano na majadiliano, kama walivyosema (Best na Kahn, 1993) njia moja wapo ya kupunguza changamoto na kuongeza ubora ni kutumia mbinu zaidi ya moja. Hivyo mtafiti ameamua kuchagua mbinu tofauti tofauti kwani kila mbinu ina ubora wake.

3.5.1 Mbinu ya Mahojiano

Mahojiano ni mbinu ambayo inatumika kukusanyia data kwa kuwahoji watafitiwa ana kwa ana, Kama walivyosema Kombo na Tromp (2006), mahojiano ni majibizano ya

ana kwa ana au ya simu, barua pepe na kadhalika yanayofanyika kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala la fulani la kiutafiti lililoainishwa.Mulokozi (1983) anaeleza kwamba mahijiano ni majibizano ya ana kwa ana au simu, kidijitali/ barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainsishwa.Nayo Kamusi ya kiswahili sanifu (2004) inaeleza kwamba mahojiano ni hali ya kuuliza maswali ili kutaka kujua maarifa au uwezo wa mtu juu ya jambo fulani.

Ni maswali ambayo mtu huulizwa na mtu au kikundi cha watu pamoja na majibu anayotoa.Kothari (1990) anadai kuwa mbinu hii inahusu mchakato wa kuuliza maswali ambapo mtafiti anafursa ya kufafanua maswali ambayo hayaeleweki na mtafitiwa / watafitiwa. Kwa mantiki hiyo mbinu hii ni mbinu ya majibizano ya ana kwa ana baina ya watu wawili au zaidi kwa njia ya simu au ya vikundi yenye lengo la kumpa taarifa muhimu mtafiti kuhusiana na mada yake (Enon, 1998) anasema ni mbinu ya kukusanya taarifa inayohusisha maswali kwa njia ya mdomo au majadiliano, mtafiti aliwahoji watu ishirini na sita (26) watu hawa waliteuliwa kwa maksudi kutokana na umahiri wao kuhusiana na mada husika, wasailiwa hawa tuliwatumia wazee (20) na wafanyakazi au wasemaji wakuu wanaohusiana na mambo ya kiutamaduni walikuwa (6).

Mtafiti ameteua njia hii kwa sababu ya kupata mawazo na mtazamo wa watafitiwa kuhusiana na majina ya mahali jinsi yanavyoakisi utamaduni kwani wazee ni watu wa zamani ambao wanaufahamu wa kutosha juu ya asili ya majin ya mahali na utamaduni kiujumla, pia wafanyakazi wa mambo ya kiutamaduni wamesomea ipasavyo mambo ya msingi yanayohusiana na uatamaduni.

3.5.2 Mbinu ya Dodoso

Mbinu hii inatumia orodha ya maswali mafupi mafupi yaliyoandikwa katika nyaraka maalumu, maswali haya hupelekwa kwa watafitiwa na kutakiwa wayajibu kisha wayarejeshe kwa mtafiti mwenyewe, majibu ya maswali haya hutumiwa kama data taarifa ya utafiti, mbinu hii iliteuliwa na mtafiti kwa sababu ya kupata ulinganifu wa majibu yatokayo kwa watafitiwa wote, mtafiti aliwatumia watafitiwa ambao ni vijana (50) wanaoishi mkoa wa Kaskazini Unguja na kuwapa karatasi zenye orodha ya maswali (16).

Maswali haya yalikuwa katika mfumo wa maswali madogo madogo na maswali ya kujielezea Miongoni mwa maswali hayo yalikuwemo yanahusu taarifa za watafitiwa wenyewe kama vile jina la mtafitiwa. Mtafiti ameteua njia hii kutokana na kupata majibu tofauti tofauti kutoka kwa watafitiwa wengi kwa wakati mmoja kwani maswali yao yote yanafanana ila majibu yanatofautiana kutoka mtafitiwa mmoja hadi mwengine, halkadhalika inaokoa muda na gharama kwani mtafiti ameweza kumuwakilisha mtu mwengine kupeleka dodoso kwa watafitiwa na yeye akaendelea na kazi zake za utafiti, pia kupata majumuisho ya majibu yote.

3.5.3 Majadiliano

Ni njia ambayo watafitiwa wanajumuika kwa pamoja, mtafiti anauliza maswali kisha watafitiwa wanajibu maswali kwa njia ya majadiliano, mbinu hii mtafiti aliitumia kwa ajili ya kupata majadiliano ya pamoja hivyo ameamua kuwakusanya vijana peke yao, na wazee peke yao, kwa siku tofauti tofauti ili wajadiliane kwa pamoja kuhusiana na mada husika, lengo la kuwakusanya kwa pamoja ni kutaka kufahamu kati ya vijana na wazee ni wapi wenye ufahamu wa kutosha kuhusiana na mada hii.

3.6 Njia ya Uchambuzi wa Data

Hizi ni njia ambazo mtafiti anazichagua kwa ajili ya kuchambulia data zake. Mtafiti ameteua njia ya maelezo. Njia hii inafaa kutumia pale mtafiti anapokusanya taarifa kuhusu mawazo ya watu, mitazamo yao, tabia zao pamoja na maswali mbali mbali ya kijamii yanayohitaji maelezo na ufafanuzi.kama ambavyo wataalamu wanavyosema kwa mfano;

Kothari (keshatajwa) anafafanua kwa kusema kuwa mkabala wa uchambuzi wa data kimaelezo huonesha jinsi watu wanavyofikiri na kuhisi juu ya kitu au jambo fulani. Mkabala huu unafaa kutumia pale mtafiti anapokusanya taarifa kuhusu mawazo ya watu, mitazamo yao, tabia zao pamoja na maswali mbali mbali ya kijamii yanayohitaji maelezo Matokeo ya utafiti huu yalichanganuliwa kwa njia ya maelezo. Maoni yote ya watafitiwa waliojibu yalikusanywa na kuchanganuliwa kwa njia ya maelezo, hivyo mtafiti alitumia njia ya maelezo kwa ajili ya kuelezea mawazo na fikra zote za watafitiwa walizoziwasilisha kwa mtafiti, kwa kueleza asili ya majina ya mahali jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu waunguja.

3.7 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpangilio maalum unaotoa mchoro kamili juu ya namna au jinsi utafiti fulani utakavyofanyika tangu hatua za mwanzo kabisa mpaka kukamilika kwake (Babbie, 1999). Zipo aina mbalimbali za usanifu wa utafiti na kwa minajili ya utafiti tunateuwa uchunguzi wa kifani kuwa aina ya usanifu wa utafiti huu. Uchunguzi kifani ni aina ya usanifu wa utafiti ambapo mtafiti huteuwa sehemu tu ya watafitiwa au vitafitiwa vilivyo vingi kwa ajili ya kuvifanyia utafiti ambavyo bila shaka vitatoa uwakilishi wa watafitiwa au vitafitiwa vyote. Katika utafiti huu mtafiti aliteuwa

baadhi ya mitaa ya mkoa wa kaskazini Unguja, ambayo iliwakilisha mitaa mingine. Pia aliteua baadhi ya watafitiwa wa mkoa huo huo na wala si watu wote wanaoishi huko ili kuwakilisha wengine katika kuchunguza etimolojia ya majina ya mahali.

3.8 Hitimisho

Sura hii inahusu mbinu mbali mbali zilizotumika katika kukusanya data Miongoni mwa mbinu hizo ni pamoja na mahojiano, hojaji na majadiliano ya pamoja, vile vile tumeelezea njia zilizotumika kuchambulia data, ambazo ni njia ya maelezo mwisho tukaelezea usanifu wa utafiti

SURA YA NNE

UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vinavyohusiana na mada yetu ambayo ni Etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja, data nyingi zilikusanywa kwa mbinu ya dodoso, mahojiano majadiliano ya vikundi, Katika mahojiano mtafiti aliwahoji wazee 20 na wafanyakazi wa mambo ya kiutamaduni 6, pia katika dodoso mtafiti aliwapa dodoso vijana 50 wa Kaskazini Unguja. Halkadhalika mtafiti aliona ipo haja ya kujadiliana kwa kina kuhusu mada yetu kati ya vijana na wazee hivyo akaamua kuweka majadiliano ya pamoja. Mbinu zote hizi zilitumika kwa ajili ya kuuliza maswali yanayohusiana na mada yetu.

Mgawanyo huu umefanyika ili kutoa fursa kwa mtafiti kuchanganua data kwa urahisi na kufanya ulinganishi wa matokeo ya watafitiwa. Uchambuzi umefanywa kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti huu. Ambayo ni mawili,lengo la kwanza kueleza asili ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja, na lengo la pili ni kujadili asili ya majina ya Kaskazini Unguja jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja, Sura hii inaanza kwa kuwasilisha data na kuzichambua data. Uwasilishaji na uchambuzi huo wa data umefanyika kama ifuatavyo:

4.2 Kueleza Asili ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Unguja

Ni kawaida kuwa kila kitu duuniani kina asili na historia yake, hakuna kitu kilchokuja kwa bahaati lazima kutakuwa na jambo ambalo limefanya kuja kwa kitu hicho, hivyo ni dhahiri kwamba hata majina ya mahali yana asili zake. Matokeo ya utafiti huu

yamedhihirisha bila ya mashaka yoyote kwamba majina ya mahali yana asili zake ambapo asilimia 96 ya watafiti wamekubaliana kuwepo kwa asili hizo, hivyo mtafiti amechanganua data katika majimbo sita ya Kaskazini Unguja ambayo ni Nungwi, Tumbatu, Mkwajuni, Kijini, Donge na Bumbwini, katika majimbo yote hayo mtafiti amechagua baadhi ya shehia zake na kuzichanganua kama ifuatavyo:

4.2.1 Etimolojia ya Mtaa wa Nungwi

Nungwi ni kimoja miongoni mwa vijiji vya miji ya Unguja. Hii ni sehemu ambayo watalii wanaipenda sana kwa sababu kuna vivutio vingi vya Utalii. Sehemu hii ipo katika jimbo la Nuungwi, Shehia ya Nungwi. Sababu ya kuitwa jina hili ni kwamba enzi za kale watu wa Zanzibar walikuwa na desturi ya kufanya mikutano yao kwenye sehemu mbalimbali za kisiwa cha Unguja. Mikutano hiyo mara nyingi ilikuwa ikifanyika kwenye sehemu maalumu ya Wilaya ya Kati. Siku moja baada ya kikao kumalizika washiriki wakawa wanaulizana kikao kingine tutakifanya wapi? Mmoja wao akajibu tutakutania hapa hapa. Kwa sababu hiyo sehemu hiyo ya mkutano ikapewa jina la ‘Mpapa’. Walipokutana mara nyeingine mtu mmoja kati yao alishindwa kuhudhuria. Mtu huyu alikuwa na kawaida ya huchukua samaki aina ya bunju ambaye anaitwa ‘Nungu’. Baada ya mtu huyu kukosekana kwenye kikao mmoja kati ya wajumbe aliuliza kwamba, yule mtu wa Nungu leo hajaja?Aliuliza hivyo kwa kuwa muhogo kwa siku hiyo ulikosa kitoweo. Baada ya kikao kumalizika neno Nungu liligeuzwa sauti yake ya mwisho likawa Nungwi. Kutokana na aina hiyo samaki ndio pakapatikana jina la Nungwi. , Maelezo haya yanayotokana na dodoso nambari 4 yakiungwa mkono na mzee mwenye umri wa miaka 79 ambaye alitowa data kama hii katika mahojiana.

Sehemu hii ya Nungwi imapakana na vijiji vingi kama vile Kisanakani, Jomba, Sazani na Kibokwa. Vijiji hivi vyote wakaazi wake walikimbia kutokana na vitimbi vya wamanga. Wamanga walikuwa wakiwabaka na kuwaigiza utumwani. Walihama vijijini mwao na kuelekeaFunguni Rasini. Huko ndiko kulikokuwa na usalama kwa kiasi. Watu wa Nungwi ni wenye asili ya kutoka Maskati, Kaskazini mwa India, Shirazi na Irani. Kwa lugha nyengine watu hawa wanatokana na mchanganyiko kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu.

4.2.2 Etimolojia ya Mji wa Kidoti

Huu ni mji mkuu wa Shehia zote za jimbo la Nungwi ukiitoa sehemu ya Nungwi wenyewe. Umashuhuri huu umetokana na shule iliyojengwa katika eneo hilo. Shule hiyo inaitwa kwa jina la shule ya Kidoti.Shule hii kwa hakika haipo kati kati ya Kidoti. Shule hii ipo mipakani baina ya Kidoti na Kilimani. Waasisi wa shule hii ni watu wa Tazaari na Kilimani. Asili ya jina hili la Kidoti ni kuwa hapo awali sehemu hiyo ilikuwa ni shamba la Mwarabu ambapo alikuwa ananunua maeneo kidogo kidogo kutoka kwa wenyeji wa eneo hilo. Mwaarabu aliendelea kununua ardhi ya mahali hapo siku hadi siku. Aliendelea kununua eneo hilo mpaka akapata eneo kubwa kiasi cha kutosha. Wenyeji wa eneo hilo wakasema Mwarabu ameuziwa kidoto tu likiwa na maana kidogo tu lakini sasa amepata eneo kubwa mno.

Hivyo kutokana na neno kidoto, ndipo wakaazi wa hapo wakabadilisha herufi ya mwisho na kupatikana jina la Kidoti Sehemu hii hapo awali ilikuwa ni msitu tu. Watu walikuwa wanaishi kilimani na Tazari. Baadae watu wakawa wanajenga kidogo kidogo mpaka kukawa na mji mkubwa. Maelezo haya yalitokana na mama mmoja mwenye umri wa miaka 82 mkaazi wa eneo la Kidoti. Alitoa maelezo haya kwa kina

wakati mtafiti alipomuhoji siku ya tarehe-12/9/2017. Pia mtafiti alipofanya mahojiano na watu mbalimbali hapo Kidoti kuna vijana watatu waliodai kwamba, walipokea maelezo kama hayo kutoka kwa wazazi wao. Watu wa Kidoti asili yao ni mchanganyiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali. Wapo wanaotoka Tanzania Bara hasa hasa sehemu za Bagamoyo.Ushahidi wa hoja hii unatokana na kuwepo kwa majina ya Jadi, Mwinyi, Mwomboka na mengineyo. Majina haya hayana asili ya uzanzibari. Halkadhalika kuna watu wanaotoka Kilimani na Tazari na maeneo mengine. Kwa upande wa mipaka kijiji hiki kwa upande wa Magharibi kimepakana na Pwani ya Kikokwe, Masharki imepakana na kijiji cha Bwereu na msitu. Kaskazini imepakana na kijiji cha Kigunda na Kusini kimepakana na Fukuchani.

4.2.3 Etimolojia ya Mtaa wa Kilimani

Mzee Bakari mwenye umri wa miaka 81 amesema kuwa Kilimani ni eneo ambalo chini upande wa Kusini Magharibi imepakana na shule ya Kidoti. Kaskazini Magharibi imepakana na barabara ya kwendea Nungwi, upande kaskazini imepakana na Tazari, Mashariki pori lisilo mpaka kusini imepakana na Kidoti. Kilimani ni sehemu ya zamani kabisa waliohamia watu. Jina la zamani ambalo linajulikana kihistoria ni Kilimani. Jina hili linatokana na ukweli kwamba sehemu hii ipo juu ya kilima. Mtu alipokuwa anaenda katika sehemu hii ni lazima apande mlima. Historia inaendelea kueleza kwamba, watu wa Kilimani na Tazari hawafahamiani kutoka na tofauti ya utamaduni wao. Inasemekana kuwa eneo hili liliitwa Kilimani kwa sababu ya neno la Kiarabu *kalimaini* ikimaanisha watu wenye kauli mbili. Watu hawa walikuwa wanafiki yaanii walikuwa na maneno mazuri wakati wanapokutana na watu wa Tazari, lakini walikuwa na maneno mabaya dhidi ya watu Watazari wanapokuwa

wenyewe kwa wenyewe. Kwa hivyo kijiji cha Kilimani kiliitwa hivyo kwa sababu Kipo juu ya Kilimani au kwa sababu ya watu wake waliokuwa na kauli mbili.

4.2.4 Etimolojia ya Mtaa wa Tazari

Tazari ni sehemu ambayo ipo katika Jimbo la Nungwi katika Shehia ya Tazari. Mipaka yake kwa upande wa kusini ni kijiji cha Kilimani, kaskazini imepakana na Chanjaani Kigunda, Mashariki Pori na Magharibi Pwani ya Kikokwe. Tazari ni sehemu ambayo imezaliwa kutoka katika kijiji cha Kilimani.

Hii inatokana na mtu mmoja aliyekuwa mwenyeji wa Kibeni kutokana na historia yake. jina hili la Tazari liliitokana na mtu mmoja aliyekuwa anaitwaa Ali Haji Dawa. Kama ilivyobainishwa hapo nyuma Ali Haji Dawa alitokea Kibeni. Bwana huyo aliowa Kilimani na alikuwa akiishi hapohapo. Alipata watoto kadhaa lakini wote walikufa kwa sababu zinazoaminiwa kuwa za kishirikiana. Inaainiwa kwamba watu wa Kilimani walimpa mke bwana huyu, lakini hawakuwa tayari kumpa fursa ya kuendeleza kizazi katika mji wao. Bwana huyu alikuwa ni mganga wa kienyeji.

Alipoona watu wa Kilimani wanamtendea vibaya alienda kuvunja Pori mahali ambapo baadae paliitwa jina la Tazari. Alijenga makaazi yake kwenye sehemu ambayo kwa sasa ina jingo la msikiti wa Tazari. Katika sehemu hiyo akaandika tangazo lililosomeka *tahadhari*. kwa maana kwamba musiiniaribie, mushanifanyia uadui mkubwa huko nyuma. Sasa hivi muniache na maisha yangu. Ni maelezo ambayo tumeyapata wakati tulipokuwa tunajadiliana kati ya wazee na vijana na wakaafikiana kuwepo kwa ukweli wa historia hii.

4.2.5 Etimolojia ya Mtaa wa Fukuchani

Jina hili la Fukuchani linatokana na asili tofauti tofauti kutokana na maelezo ya baadhi ya watafitiwa. Mzee Faki mwenye umri wa mika 77 ameeleza kuwa asili ya mtaa wa Fukuchani ni msafara wa raisi wa kwanza wa Zanzibar mzee Abeid Amani Karume., Jina hili liliibuka pale Karume alipokuwa anakwenda Nungwi kwa ajili ya kampeni za kisiasa. wakati walipokuwa kwenye gari walikwamakwama kwenye sehemu hii. Gari zote zililazimka kusimama kwa sababu palikuwa na mchanga mwingi. Mzee Karume alisema hapa palipobakia tuteremke na twende kwa miguu kwa sababu ya fukucha na ndipo likapatikana jina hili la fukuchani.

Bi Mwanaidi mwenye umri wa miaka 72 yeye ameeleza kwamba jina la Fukuchani linatokana na mashindano ya mbio yaliyofanyika sehemu hii. Watu walikuwa wakishindana kumtafuta atakayefika mwanzo kileleni., katika mashindano hayo wengine walipita juu sehemu ambayo haina mchnga mwingi na wengine wakapita chini sehemu yenye mchanga mwingi. Wale ambao wamepita juu wameshinda na wale waliopita chini wameshindwa. Kushindwa kulitokana na kupita kwao kwenye sehemu iliyokuwa na mchanga mwingi. Walioshindwa walijitetea kwa kusema kwamba tumefika mwisho kwa sababu wakati tunapiga mbio miguu yetu ilikuwa inapata fukucha la michanga.

Kwa sababu hiyo tulikuwa wazito wa kutembea na ndio maana likapatikana jina la fukuchani. Asili ya watu wa fukuchani ni kutoka Bagamoyo, kwa kuwa sehemu ipo karibu na pwani hivyo watu wa Bagamoyo walikuwa wanapapenda sana kutokana na shughuli zao za uvuvi. Walikuwa wanafika hapo na kukaa muda mrefu na baadae kuhamia na kufanya makazi yao ya kudumu.

4.5.6 Etimolojia ya Kijiji cha Tumbatu

Kijiji cha Tumbatu kipo wilaya ya kaskazini A, mkoa wa kaskazini Unguja. Asili ya watu wa Tumbatu ni kutoka shirazi na Tanga. Sehemu zote za kijiji hiki zimepakana na bahari. , Kwa upande wa asili ya jina la Tumbatu kuna mitazamo kadha wa kadha. Mtazamo uliomashuhuri na unaoaminika zaidi ni ule wa watafitiwa ambao ulitokana na dodoso 10 na wasailwa 2 unasema kwamba asili ya jina hili ni kwamba watu wa Tumbatu ni wa mwanzo kujenga madau. Watu hawa walitoka visiwani kwenda Tanga katika sehemu inayoitwa kisiwa mwana Unguja. Wakaulizwa na wenyeji wao Wazigua hapa nyie mmekujia kwa nini? Wakimaanisha chombo gani? Kwani wakati huo kulikuwa hakuna chombo chochote cha kuvusha. Wale watu wakajibu tumekuja na tumba tupu, likiwa na maana ya chombo walichokitumia. Hapo ndipo pakapatikana jina la Tumbatu kutokanaa na neno ‘tumba tupu.

4.2.7 Etimolojia ya Kijiji cha Mkokotoni

Ni miongoni mwa sehemu za makazi za watu iliyopo karibu na bahari. Mkukotoni ni bandari yashughuli zote za uvuvi. Halkadhalika wasafiri wa maboti, vidau na ngalawa hufanya safari zao kuanzia hapo. Mkokotoni ipo wilaya ya Kaskazini A katika jimbo la Tumbatu shehia ya Mkokotoni. Kwa mujibu wa Bi Maryam kijiji hiki kilipewa jina hili la Mkokotoni kwa sababu hapo zamani kulikuwa na kituo cha polisi. Kwa wakati huo mtu akifanya kosa huambiwa watu wengine kwamba mkokoteni mpelekeni kituo cha polisi. Akifika huko anapewa adhabu inayomstahikia. Eneo hilo pia lilikuwa na mahakama na jele ya kufungwa watu. Kutokana na neno mkokoteni ndipo kukapatikana jina la mahali na pakaitwa mkokotoni. Kwa sasa kituo hicho cha polisi kimehamishiwa eneo jirani na lile jengo la mwanzo limefanywa banda la kuuzia

samaki. Hata hivyo jina la mkokotoni bado lipo., Mipaka ya kijiji hiki ni Mashariki kimepakana na kijiji cha Kivunge, Magharibi kimepakana na Mto wa Pwani, kaskazini kimepakana na bahari, na Kusini kimepakana na Mkwajuni.

4.2.8 Etimolojia ya Mtaa wa Muwanda

Ni mtaa maarufu sana katika jimbo la Tumbatu ambao upo katika shehia ya Muwanda. kwa maelezo ya kijana mmoja katika dodoso, anadai kwamba, alipokea kutoka kwa babu yake kuwa kijij hiki kilikuwa na bandari inayofikiwa na wavuvi kutoka huko Bara. Katika bandari hiyo kulikuwa na majahazi makubwa. hapo zamani kijiji hiki kilikuwepo chini ya ufukwe wa bahari. Ngalawa zilikuwa zinafungwa chini ya nguzo za nyumba kutokana na kukaribiana sana baina ya bahari na makazi ya watu. Baadae watu waliamua kuhama na kuja sehemu ya juu ya ufukwe ambapo maji ya bahari hayafiki Sehemu hiyo ya juu kulikuwa na muwanda mkubwa na ndio sababu ya kupatikana jina hili la muwanda. Mtaa huu kwa upande wa kusini umepakana na mtaa wa Bumbwini. kaskazini kuna mtaa wa Pale, Mashariki kuna Muwanda na Mgharibi kuna Bahari. Asili ya watu wa Muwanda ni mchanganyiko kutoka sehemu mbali mbali kama vile Tanga, Chaani na Bumbwini.

4.2.9 Etimolojia ya Mtaa wa Pale

Pale ni i mtaa ambao upo katika jimbo la Tumbatu, shehia ya Pale, Mtaa huu umepakana na mtaa wa Mto wa Pwani kwa upande wa kaskazini, Kusini umepakana na Kipange, Mashariki umepakana na Kingole na Maghaibi umepakana na bahari. Maelezo ya dodoso nambari 5 na majadiliano yaliyofanywa baina ya mtafiti na mtafitiwa yanasema jina la Pale limepatikana kwa sababu sehemu hii ipo juu ya

kilima. Watu waliokuwa wanaokwenda sehemu hiyo walipokuwa wakiulizwa munakwenda wapi? Walikuwa wanasema tunakwenda pale, huku wakionesha mikono yao kwenye kile kilima. Kwa muktadha huu sehemu hii ikaitwa Pale Asili ya watu wa Pale ni kutoka Tumbatu. Baadhi yao wanaotoka Mkwajuni, Mtambile na Karange.

4.2.10 Etimolojia ya Mtaa wa Mchangani

Mtaa huu upo karibu sana na Jimbo la Donge. Hata hivyo katika mgawanyo mpya wa Majimbo mtaa huu umeingizwa katika jimbo la Tumbatu. Sababu ya kupatikana kwa jina hili ni kwamba katika mtaa wa donge kulikuwa na udongo mwekundu, Udongo huo uliishia mahala fulani palipokuwa njia panda. . Sehemu inayofuata udongo wake ni mweupe ambao upo kama mchanga mchanga. Kwa muktadha huo ndio maana sehemu hii ikapewa jina lake la Mchangani. Mtaa huu umepakana na mtaa wa Kipange kwa upande wa kaskazini, Mbiji kwa upande wa kusini mashariki kuna Donge na Magharibi kuna Muwanda. Asili ya watu wa Mchangani ni kutoka Mtambile, Donge na Matemwe. Taarifa hizi ni kwa mujibu wa mzee Ali Faki anaeishi katika mtaa huu.

4.2.11 Etimolojia ya Mtaa wa Mkwajuni

Mkwajuni ni mtaa maarufu sana kutokana na kuwepo kwa shule ya zamani sana ambayo ipo barabarani. mwalimu mmoja ambaye pia ni mzee wa mtaa huo alipohojiwa kuhusiana na asili ya mtaa huu amesema kwamba mtaa huu umepewa jina hili la Mkwajuni kutokana na kuwa hapo zamani kulikuwa na mti mkubwa ambao ulikuwa unaitwa mkwaju. Pembezoni mwa mti huo kulikuwa na soko kubwa ambapo watu walikuwa wanakusanyika hapo na kufanya biashara zao za kijamii. Hilo lilikuwa

ni soko la biashara ndogondogo kama vile nazi, mchele, muhogo, viazi, matunda nakadhalika. na Pia hii ilikuwa ni sehemu ambayo mtu alipokuwa akifanya utovu wa adabu hukamatwa. na kupigwa vipo kwa kutumia bakora zinazotokana na mti huo wa mkwaju. Kama tulivyosema hapo awali ni kwamba mtaa huu ni maarufu sana. Wazee wa zamani wa eneo hili wanapokuwa na vikao vyao vinavyohusiana na mambo yao ya kijamii kama vile msiba, harusi nakadhalika vilikuwa vinafanyika katika sehemu hiyo. Asili ya watu wa Mkwajuni ni mzunguko wa kuhama na kuhamia kwa watu kutoka kanda za pwani na kisiwani Tumbatu. Mipaka ya mtaa huu ni Chutama kwa upande wa kusini. Kwa upande wa Kaskazini kuna kijiji cha Kivunge. Upande wa Mashariki Mkwajunini imepakana na Kidombo na Maghharibi imepakana na Pwani pamoja na Mkokotoni.

4.2.12 Etimolojia ya Mtaa wa Moga

Moga ni mtaa ambao upo katiika Jimbo la Mkwajuni katika shehia ya Moga. Mipaka ya mtaa huu kwa upande wa kusini ni Chaani Masingini, kaskazini kuna mtaa wa Chutama, magharibi imepakana na Donge na mashariki imepakana na Gamba. Asili ya kupatikana kwa jina hili ni kwamba, hapo awali katika sehemu hii kulikuwa na watu wanatisha sana. Wanajamii walikuwa wanawakimbia watu hao kwa sababu walikuwa wanawaogapa. Kila mtu aliyekuwa akiishi eneo hilo alikuwa ni Moga. Kwa sababu hiyo pakapatikana jina la Moga.

Vile vile dodoso nambari 6 linaloeleza asili kuhusiana na jina la Moga lilisema kuwa sehemu hii iliitwa hivi kwa sababu wenyeji wake walikuwa wanaambizana kwamba mtu aliyekuwa ana woga basi hapa asije, Kwa asili watu wa Moga ni watu kutoka Tumbatu na Matemwe.

4.2.13 Etimolojia ya Mtaa wa Matemwe

Matemwe ni mtaa uliopo katika Jimbo la Mkwajuni katika shehia ya Matemwe. jina hili la Matemwe lilitokana na watu waliohamia katika sehemu hiyo. Wakati walipohamia kwa mara ya kwanza watu hawa walikuta pori tupu na wakaamua kujenga vibanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuishi katika sehemu hiyo, Hawakujua sehemu hiyo waipe jina gani. Waliulizana sehemu hii tuipe jina gani? Hivyo kila mtu akawa anasikilizia kwa kutega sikio lake kwa makini. Mmoja wao akatema mate poh! na kuombwa paitwe Matemwe kama alivyotema Mate.

Kila mmoja akaliafiki jina hilo, na ndio mpaka leo pakaitwa Matemwe. Awali palikuwa na vijumba vidogo vidogo lakini kila mda unapokwenda watu wanazidi kujenga majumba makubwa makubwa. Sasa hivi Matemwe, umekuwa mtaa mkubwa wenye majumba makubwa, Sasa hivi una shule na hospitali pamoja na mahoteli mengi makubwa makubwa kwenye fukwe zake. Mtaa huu umejengwa na vjiji vidogo vidogo kama vile Mbuyu tende, Kachongwa, Mwangaseni, Mbuyu popo nakadhalika. Asili ya watu wa Matemwe ni kutoka Tanzania Bara. Haya ni maelezo yaliyotolewa wakati wa mahojiano ya pamoja yaliyofanyika tarehe 15/8/2017.

4.2.14 Etimolojia ya Kijiji Gamba

Kijiji hiki kipo katika wilaya ya Kaskazini A katika jimbo la Mkwajuni,, shehia ya Gamba. Vijana watatu katika dodoso zao pamoja na wazee wawili wakati wa usaili walisema kijiji hiki cha Gamba asili ya jina lake ni kuwa hapo zamani kulikuwa na mtu anayeitwa Msaduchi. Mtu huyo alikuwa na kibri, shujaa, mwenye jeuri Pamoja na sifa hizo pia alikuwa anajiona na kujisikia sana. Watu walikuwa wanamuogopa sana kwa sababu alikuwa anapenda sana kuwaonea. Ilikuwa hata kama mtu atapita na

mke wake anamchukua na hawezi kusema lolote. Watu walikuwa wanamkimbia lakini wakikaa pekee yao wanasema hawamuogopi. Mtu mmoja akawauliza mbona nyie munamkimbia Msaduchi wakati munaapokaa peke yenu mnajiigamba na kusema hammuuogopi? Kutokana na neno munajigamba sehemu hii ikaitwa Gamba.

4.2.15 Etimolojia ya Mtaa wa Chutama

Huu ni mtaa ambao upo karibu na mtaa wa Gamba. Huu ni mtaa ambao upo katika shehia ya Chutama jimbo la Mkwjuni, ambapo watafitiwa 7 walisema kwamba asili ya jina hili la chutama linatokana na historia ya Gamba. Imekwisha kufafanuliwa kwamba walikuwepo watu ambao wanamuogopaMsaduchi kutokana na sifa zake kama ilivyokwishaelezewa kwenye (4.2,15). ya kwamba wale watu wanaomkimbia walipofika sehemu hii wanajificha lakini kujificha huko ni kwa kuchutama. Walijificha ili wasionekane na Msaduchi. Kwa sababu hiyo ndio maana pakaitwa Chutama.

4.2.16 Etimolojia ya Kijiji cha Kinyasini

Kinyasini ni kijiji kilicho katika shehia ya Kinyasini. Mashariki kimepakana na kijiji cha Kisongoni, magharibi kijiji cha Banda maji, kusini kimepakana na kijiji cha Mdodo pilau na kaskazini kimepakana na kijiji cha Kikobweni. Sababu ya kijiji hiki kupewa jina la Kinyasini ni kuwa katika sehemu hii palikuwa na miti mikuubwa kama vile mipopo na pia palikuwa nyasi. Kutokana na nyasi hizo ndizo zilizopelekea sehemu hiyo kuitwa Kinyasini.

4.2.17 Etimolojia ya Kijiji cha Kibeni

Kijiji hiki kipo katika wilaya ya Kaskazini A katika shehia ya Kibeni. Mtafiti alifika sehemu husika na akakutana mzee mwenye umri takriban miaka 79 na akamhoji

kuhusiana na jina la kijiji hicho. Yule mzee hakusita na alisema jina hili lilitokana na kwamba hapo zamani kulikuwepo na watu ambao wanapora vitu vya watu; yaani wanaiba. Kuna siku moja katika pirika zao za kuiba wakakaa kujadiliana mmoja wao akauliza leo kiibwe nini? Mmoja akasema kiibwe kikombe tele, yaani waibe kikombe kilichojaa shilingi tele. Kwa muktadha huu ndio pakapatikana jina la Kibeni. Kijiji hiki kwa upande wa Mashariki kimepakana na Kijiji cha Kidombo, magharibi kimepakana na Kivunge, kaskazini kimepakana na Muwange na kusini kimepakana na Uyagu.

4.2.18 Etimolojia ya Kijiji cha Kivunge

Kijiji hiki kipo katika Wilaya ya Kaskazini A katika jimbo la Mkwajuni., Hiki ni kijiji ambacho kimepakana na Pitanazako kwa upande wa kaskazini, halkadhalika upande wa kusini kimepakana na Mkwajuni, mashariki kijiji cha Kibeni na magharibi kimepakana na kijiji cha Mkokotoni. Mtafiti alipochunguza asili ya kijiji hiki amepata mitazamo tofauti kwa watafitiwa wake. Kijana mmoja ambaye amepokea kutoka kwa babu yake, amesema kwamba asili ya jina hili la Kivunge ni kwamba hapo zamani wazee wa zamani mambo yao walikuwa wanayavungavunga. Yaani walikuwa wakiyavungavunga mambo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, na kiutamaduni. Kutokana na tabia hii ya kuvungavunga mambo kijiji hiki kikaitwa Kivunge.

Lakini mtazamo mwengine ni ule wa baadhi ya wazee. Mtafiti alipata fursa ya kuwahoji kama wazee 5 ambao walisema kwamba, asili hasa ya jina hili la Kivunge ni kuwepo kwa mtu na mke wake ambapo mume anapopata hakiba yake anampa mke wake na yule mke anaiweka hakiba ile kwenye kitambaa ambacho kimevungwa. Ilitokeaa siku moja kuna sehemu kunauzwa ardhi, yule mume akamwambia mke wake

kalete kile kivunge tununue ile ardhi. Kutokana na hali hiyo ndipo mahali hapo pakaitwa Kivunge. Mintarafu ya hayo kuna mzee mmoja alipohojiwa na mtafiti kuhusiana na jina hili la Kivunge amesema kwamba asili ya jina hili lilitokana na watu ambao wanaiba. Baada ya kuiba walikuwa wanakivunga kile walichokiiba ili kisionekane na ndio maana sehemu hii ikaitwa kivunge., mtafiti amebaini kwamba mtazamo ambao ulionekana kuwa na nguvu ni mtazamo wa pili kwa sababu umeungwa mkono na watafitiwa asilimia 60% ukilinganisha na mtazamo wa kwanza na watatu.

4.2.19 Etimolojia ya Kijiji cha Pitanazako

Hiki ni kijiji ambacho kipo karibu sana na kijiji cha Kibeni. Hiki ni kijiji ambacho mtafiti aligundua kuwa kutokana na kukaribiana kwake na Kibeni hata historia zake zimefanana au ni mwendelezo wa historia ya Kibeni iliyoelezwa hapo juu. Inasemekana limepatikana jina hili la Pitanazako kutokana na hao watu waliokuwa wanaiba vitu vya watu. Katika harakati zao hizi, kulitokea watu wengine ambao wanawatafuta hawa wezi baada ya kuwaona tu wakaoneshana vidole na kusema wale pale wezi., Wale wezi walipowaona wakawambia haya hayawahusu Pitanazako, mushike adabu zenu musishughulikie ya watu. Kutokana na jina hili la Pitanazako. Kwa upande wa mipaka yake kijiji cha Pitanazako kimepakana na Kibeni kwa upande wa mashariki, magharibi kimepakana na Shangani na Bahari, kaskazini Potoyana kusini kimepakana na Kivunge.

4.2.20 Etimolojia ya Kijiji cha Muwange

Muwange ni neno linalotokana na kuwanga, likiwa na maana ya imani za kishirikina. Huu ni mtaa ambao upo wilaya ya Kaskazinii A katika shehia ya Muwange. Muwange

ni kijiji ambacho kimepakana na Potoya kwa upande wa kaskaziini na kwa upande wa kusini kimepakana na Kivunge. Kijiji hiki kwa upande wa mashariiki kimepakana na Mwambakilini na magharibi Pitanazako., Mtafiti alipohoji kuhusiana na historia ya jina hili la Muwange aliambiwa limetokana mtu na ambaye aliibiwa vitu vyake. Baada ya kuwauliza watu kuhusiana na uibwaji huo wa vitu vyake watu wakwamwambia hawajui.

Hata hivyo watu wakamshauri labda ‘muwange’. Mtafiti alipohoji kuhusiana na maana ya neno hili alipata mapokezi mawili tofauti. Kuna ambao wamesema lina maana ya kupiga ramli yaani kutazamia katika uganga wa Kienyeji. Wapo waliosema kuwa muwange yaani hao waloiba kazi zao ni za kuvunja mawe. Mapokezi yote haya tumeyapokea kutoka kwa watafitiwa. Hata hivyo asilimia 70% ya watafitiwa wanasema lina maana ya kupiga ramli. Na hiyo kwa kweli ndio kauli yenye nguvu na hiyo ndio sababu kubwa sehemu hiyo kuitwa Muwange.

4.2.21 Etimolojia ya Mtaa wa Bumbwini

Ni mtaa maarufu sana ambao upo katika Wilaya ya Kaskazini B ambapo asili ya watu wake ni kutoka Bara. Asili ya jina la Bumbwini kutokana na taarifa zilizojazwa kwenye dodoso na vijana na majibu ya usaili yanayotokana na kuhojiwa wazee jina hili linatokana na vitimbwi vya akina mama wa zamani. Enzi hizo watoto wakiume walikuwa wakifanyiwa tohara katika jando badala ya Hospitali. Ikifika siku ya kutoka wanafanyiwa shughuli kubwa. Katika shhughuli hizo kina mama wanapopeta mchele, chenga wanaweka pembeni. Baada ya hapo wanaenda sehemu kutwanga chenga hizo na na kutengeneza bumbwi. Kutokana na hilo bumbwi ndio pakaitwa Bumbwini.

4.2.22 Etimolojia ya Mtaa wa Misufini

Misufini ni mtaa maarufu sana. Mtaa huu ndio kitovu cha eneo la Bumbwini. Huu ni mtaa ambao upo pembezoni mwa shule kongwe na shule ya mwanzo katika jimbo la Bumbwini. Awali shule hii ilikuwa inaitwa shule ya Misufini lakini baadae ikabadilishwa jina na kuitwa shule ya Bumbwini. Mahali hapo pameitwa Misufini kutokana na misufi mingi ilyokuwepo sehemu hiyo.

Kwa hivi sasa misufi hiyo haipo tena lakini jina bado lipo. Kijiji cha Misufini kwa kusini imepakana na Bahari, kaskazini kimepakana na Shehia ya Makoba, maghaaribi kuna Mangapwani na mashariki kuna Mahonda Asilli ya watu wa Misufini ni kutoka Tumbatu. Hoja hizi zilizjengwa na mtafiti zinatokana na i maelezo kutoka katika madodoso nambari 10 ya vijana.

4.2.23 Etimolojia ya Mtaa wa Makoba

Ni mtaa ambao upo katika wilaya ya Kaskazini B Jimbo la Bumbwini,katika shehia ya Makoba ni mtaa maarufu sana kisiwani Unguja, katika mahojiano ya pamoja tulipata sababu ya kuitwa Makoba ni kwamba kulikuwa na mzee mmoja alikuwa anabeba mkoba pindipo anapokwenda misufini kwa ajili ya mahitaji ya nyumbani kwake, hivyo kulikuwa na njia kila siku anapita, sehemu hiyo kulikuwa na wazee wanakaa ambapo walikuwa wanacheza bao, hivyo yule mzee alikuwa akipita hapo na mkoba wake anaitwa na wazee wenzake mzee Makoba anaitikia na kwenda kuwasilimia na kuondoka na ndio maana pakapatikana jina la Makoba, mtaa huu umepakana na Mafufuni kwa upande wa kaaskazini, kusini kuna Misufini, upande wa Magharibi kuna Bahari,na Mashariki kuna Donge

4.2.24 Etimoojia ya Mtaa wa kidazini

Ni mtaa ambao upo katika Jimbo la Bmbwini, ni mtaa ambao upo karibu na Misufini kwa upande wa Kaskazini, halkadhalika umepakana na kijiji cha Manngapwani kwa upande wa Kusini, Mashariki kuna Mahonda na Magharibi kuna Bahari, Bi Mwajuma anasema kuwa limepatikana jina hili la Kidazini kutokana na kuwa hapo awali kulikuwa na mtu anaemiliki sehemu hiyo ambayo ilikuwa ni shamba kubwa, mtu huyu aliamuua katika shamba hiyo kupanda michungwa na midanzi mingi, baadae watu wakaanza kujenga nyumba pembezoni mwa lile shamba, hivyo kutokana na kuwepo kwa ile michungwa na midanzi ndio likapatikana jina la Kidanzini.

4.2.25 Etimolojia ya Mtaa wa Mkungwa

Ni mtaa ambao upo katika wilaya ya Kaskazini B katika jimbo la Bumbwini, jina hili la mkungwa kwa mujibu wa maelezo ya mzee Faki anasema lilipatikana na kuwa hapo zamani kulikuwa na mambo ya vijana yaani wasichana na wavulana hivyo wale wanawake walikuwa wanachukua vyakula kwenye mkungu walikuwa wanawapelekea wavulana wao, watu wnaokwenda sehemu hiyo hupewa tahadhari mapema kwamba ukienda huko usije ukachukua mkungwa, na ndio maana pakapewa jina hilo, mipaka ya mtaa huu ni kwamba kwa upande wa Kaskazini kumepakana na kijiji cha Kioneni, Kusini kumepakana na Kijiji cha Majibweni na Magharibi kumepakana na Pangani.

4.2.26 Etimolojia ya Kijiji cha Jitenge

Wanajamii wa jamii hii asili yao ni kutoka Tazari, katika eneo hili walikuja wakavunja pori na kuamua kuishi hapa, ni sehemu ambayo watafitiwa wengi walikuwa wanaifahamu asili yake kwani mtafiti katika njia zote alizotumia alipata asili ya jina hili ni watafitiwa 15 walisema kwamba asili ya kupatikana kwa jina hili ni

kwamba hapo zamani kulikuwa na watu wawili mtu na nduguye,watu hawa waliamua kuondoka sehemu wanayokaa na kuamua kuvunja pori katika sehemu hii na kuishi hii ni kutokana na kuwa huko wanakotoka kulikuwa kuna ugomvi ambao haumalizi, ndipo waliposema kwamba sisi tunakwenda huko kujitenga peke yetu tunawaachia mji wenu, ni sehemu ambayo ipo katika jimbo la Bumbwini, Kaskazini yake imepakana na kijiji cha Mikweni, Kusini kuna Kilimani, Magharibi Mwembe Mtungi na Mashariki kuna Jongoe.

4.2.27 Etimolojia ya Kijiji cha Mangapwani

Kijiji hichi kipo katika wilaya ya Kaskazini B, kijiji hichi kipo shehia ya Mangapwani, asili ya watu wa kijiji hichi ni kutoka Kongo na Rufiji, katika dodoso na mahojiano ya pamoja tumepata kujua asili ya kijiji hichi cha Mangapwani ni kuwa walikuja wapashia Tumbatu sehemu inayoitwa Makutani wakajenga msikiti wenye vibula viwili, watu hao walikuwa na madema yao wakati huo na walikuwa wanaendeleza biashara zao, lakini wakipita Waswahili sehemu hiyo wanawakamata na kuwachukua na kuwafanya watumwa mpaka siku wakirudi makwao wanawachukua, hivyo watu wakahofishwa musiende huko pwani kuna wamanga wanakamata watu ndio maana pakaitwa Mangapwani.

4.2.28 Etimolojia ya Mtaa wa Mtoni

Ni mtaa ambao upo katika jimbo la Donge katika shehia ya Mtoni asilimia 70 ya watafitiwa wamesema asili ya mtaa huu wa Mtoni ni kuwa sehemu hii imetwa hivi kwa sababu kulikua na mto mkubwa katika eneo hilo, kutokana na mto huo watu wlikuwa wanaenda mtoni kukinga maji, wengine wanaenda kufua,wengine wanaenda kuoga, hivyo ikasababisha sehemu hiyo kuitwa mtoni, sehemu hii Kaskazini

iimepakana na Donge Kipange, upande wa Mashariki imepakana na Chaani na Moga, kwaupande wa Kusini imepakaa na Kijibweni na kwa upande wa Magharibi imepakana na Donge Mtambile, ama kwa asili ya watu wanaoishi sehemu hii wanatokana na watu mchanganyiko, watu wa mtoni na watu wa Tumbatu.

4.2.29 Etimolojia ya Kijiji cha Mtambile

Hiki ni Kijiji maarufu kilichopo katika Jimbo la Donge Shehia ya Mtambile. Mtafiti alimuhoji mama mmoja anayeitwa Bi Moza, ambaye alisema kwamba, kupatikana kwa jina hili la Mtambile ni kwamba kulikuwa na ugomvi wa ndugu ambao walikuwa hawapatani hata kidogo. Kutokana na hali hiyo ikabidi watu wazima waamue ugomvi huo mmoja wao akasema ndugu mtambile ikiwa na maana kila ndugu akae kando. Yaani kila mmoja akaishi sehemu yake na ndio maana pakapatikana jina hili la mMtambile. Mipaka ya kijiji hiki ni kwamba kaskazini kimepakana na kijiji cha Kipange, kusini imepakana na mtaa wa Donge, Mashariki kimepakana na Chaani na magharibi kuna Donge Mtambile.

4.2.30 Etimolojia ya Mtaa wa Vijibweni

Kama ijuulikanavyo, kisiwa cha Unguja ni kisiwa ambacho watu wake wengi ni kutoka ardhi ya Bara. Watu wengi wanapotoka huko wanafikia katika kisiwa cha Tumbatu. kwa vile Tumbatu ni kisiwa hivyo watu waliofikia hapo hawakupendelea kukaa katika kisiwa kutoka na na shughuli zao za kilimo. hivyo wakaamua kuhama na kwenda Donge na Mkwajuni. wale waliokwenda Donge, wakafikia katika ardhi ambayo ilikuwa na vijibwe vingi. vijibwe kwa Kiswahili fasaha ni vijiwe. Sehemu hii ikajuulikana kwa jina la Vijibweni. Watu wa mwanzo kuhamiia sehemu hii ni watu

wa Bara sehemu ya Bagamoyo. Mipaka ya kijiji cha Vijibweni kwa upande wa kaskazini ni mtaa wa Mtambile. kusini kuna mtaa wa Karange, mashariki Chechele na magharibi majenzi. Haya ni. maelezo yaliyotolewa na vijana watatu katika dodoso zao.

Katika kukamilisha lengo la kwanza ambalo lilikuwa ni kuchambua majina ya mahali ya Kaskazini Unguja, pia mtafiti alipochambua data zake kwa kina alibaini kwamba kuna baadhi ya majina ya mahali yanapewa majina hayo kulingana na miti au mimea, watu mashuhuri, vyakula na hata baadhi ya wanyama, kama ambavyo kuna baadhi ya watafiti waliofanya majina ya mahali pia wamegundua majina hayo kwa hivyo mtafiti aliamua kuyatenga majina haya kama ifuatavyo;

4.3 Majina ya Mahali Yanayofanana na Mimea au Miti

Haya ni majina ya mimea ambayo yamepewa majina ya mahali kutokana na kuwepo kwa mimea hiyo. kwani hata Zubeir (2015) katika kazi yake aliyochunguza etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Pemba kuwa Utambulisho wa Wapemba aligundua kuwa kuna majina ya mahali yanayotokana na miti iliyopo katika maeneo. Mfano wa maeneo hayo kama vile Mitiulaya, Mzambarau Takao, Mianzini Mharitani, Mbuyu gowe nakadhalika. Zuberi (keshatajwa) na akagundua kwamba majina hayo ya maeneo yanatokana na miti hiyo. , Mtafiti nae baada ya kuwahoji watafitiwa wake amegundua majina kama haya kama ifuatavyo:

4.3.1 Etimolojia ya Jina la Mwembe Mweupe

Mwembe ni jina la mti mkubwa kama ambavyo linavyojuulikana. lakini hata hivyo limegeuzwa kuwa jina la mtaa kutokana na historia yake. Mzee mmoja anayeishi

katika kijiji hicho alisema kwamba, sababu ya mtaa huu kupewa jina hili ni kwamba sehemu hiyo kulikuwa na muwembe ambao unazalisha embe ambazo zilkuwa na ukavu ukavu na pia zilikuwa nyeupe hata kama ni mbivu. Embe hizo zikiwa changa, mbichi, au mbivu zilikuwa nyeupe na tamu. , Kwa sababu hiyo muembe huo ukaitwa mwembe mweupe na mahala hapo napo pakaitwa Mwembemweupe Eneo hilo lipo katika wilaya ya Kaskazini A, mkoa wa kaskazini Unguja.

4.3.2 Etimolojia ya Mzambarau Machoka

Mzambarau ni jina la mti ambalo liimepewa jina la mtaa. Asili ya sehemu hii kupewa jina hili ni kuwa wakati huo watu wanaotoka Nungwi, Kidoti, Tazari wanapotoka kuuza samaki, walikuwa wanatembea kwa miguu. Walikuwa wakitembea kwa miguu kwa sababu wakati huo kulikuwa hakuna gari. Walikuwa wanatembea na wakifika fulani palipokuwa na Mzambarau walikuwa wanaweka masusu yao ya samaki na madagaa halafu wanapumzika kupunguza machoka. Kutokana na sababu hii mahali hapa pakaitwa Mzambarau machoka.

4.3.3 Etimolojia ya Kijiji cha Mwambale Mbalunguni

Hikii ni kijiji ambacho kipo wilaya ya Kaskazini A katika jimbo la Nungwi, Shehia ya Kilindi, kwa upande wa historia ya kijiji hichi sheha wa shehia ya Kilindi alisema kwamba, hapo mwanzo wazee wa Mwambale walikuwa maisha yao ni Wakilindi, baada ya watu kugombana hivyo mkubwa wa Wakilindi mzee Mwalimu Mwavura Jabu alikutwa na matatizo makubwa juu ya Kiweshu Kilindi, hivyo ikabidi amfuate sheha wake anayeitwa mzee Kidogo kutoka Nungwi, na akampa malalamiko yake na akamwambia, ‘bwana nimekuja sheha wangu nimekutwa na matatizo makubwa naomba unitafutie sehemu pakukaa’ akamwambia nisubiri Kisimani siku ya Alhamisi

nitakupa sehemu ya kukaa, hivyo siku ilipofika sheha akampelele mpaka kijiji kimoja kilichopo Nungwi sehemu hiyo kulikuwa na mbalungi mdogo, akamwambia ishi hapa na familia yako, yule mtu akasema nishapokea hapa mahali mwambale, ni sehemu yangu mali yangu, nawambia watu jirani munaokuja hapa musinikaribie muwe mbali, na ndio maana pakapatikana jina la Mwambale Mbalungini.

4.2.35 Etimolojia ya Kijiji cha Kinyasini

Ni miongoni mwa kijiji ambacho kipo katika jimbo la Bumbwini, kijiji hichi Mashariki kimepakana na kijiji cha Kisongoni, Magharibi kijiji cha Banda maji,Kusini kimepakana na kijiji cha Mdodo pilau na Kaskazini kimepakana na kijiji cha Kikobweni, sababu ya kupewa jina hili la kinyasini ni kuwa katika sehemu hii palikuwa na miti mikuubwa kama mipopo na nyasi, hivyo kutokana na nyasi hizo ndipo kulipopelekea sehemu hiyo kuitwa Kinyasini watafitiwa takribani 20 walisema hivyo.

4.2.36 Etimolojia ya Mtaa wa Mafufuni

Ni mtaa maarufu sana katika wilaya ya Kaskazini B katika jimbo la Bumbwini, ni mtaa ambao umefananishwa na mti ambao unatokana na jamii ya mnazi hii ni kutokana na kuwa sehemu hii kulikuwa na mnazi ambao uilikuwa unazaa nazi kama mavungwi, hivyo nazi hizi zilikuwa zinajuulikana kwa jina la mafufu, nazi hizi zilikuwa zinatumika kwa ajili ya kupika mafuta, na yanatumika kwa ajili ya kujipaka,kutokana na hivyo ndio pakapatikana jina la mafufuni.

4.2.37 Etimolojia ya Jina la Mzambarau Mbata

Pia hili ni jina la mtaa ambalo lipo Kaskazini B ambalo limepewa jina hili kutokana na kuwa katika hiyo sehemu kulikuwa na tanuri na mzambarau, ambapo waarabu

walikuwa kazi yao ni kukodi mashamba ya minazi, halafu huchuma nazi na kuzifanya mbata, na sehemu ambayo wanaanika nazi hizo kwa ajili ya kuzifanya mbata ni hapo kwenye huo mzambarau, baada ya kukauka nazi hizo wanazitia kwenye magunia na kuzisafirisha nje ya nchi kwa ajili ya mauzo, na ndio maana pakaitwa Mzambarau mbata.

Majina ya Mahali Yanayofanana na Vyakula

Pia kuna majina ya mahali yanayofanana na vyakula hii ni kutokana na kuwepo kwa vyakula hivyo sehemu hiyo, hata Zubeir (2015) kashatajwa amebaini kuna vyakula ambavyo vimepewa majina ya mahali kwa mfano njuguni ni jina la mahali lilitolewa kutokana na kuwepo kwa njugu yaani karanga katika eneo hilo, hivyo mtafiti nae baada ya kupata dodoso na kuwahoji wazee aligundua kuwepo kwa majina hayo kama ifuatavyo**;**

4.2.38 Etimolojia ya Jina la Mdodo Pilau

Hili ni miongoni mwa majina ya mitaa ambalo limepewa jina la vyakula, pilau ni chakula mashuhuri, ambacho hupikwa katika mashughulini, sababu ya kuitwa kwa jina hili ni kwamba, hapo zamani kulikuwa hakuna utaratibu wa kupika pilau kukiwa na shughuli, lakini baadae wakabadlisha utaratibu huo na kuanza kupika pilau sehemu yenye mdodo, tena lilikuwa linapikwa mpaka linabaki, kwa maana hiyo ndio maana pakapewa jina hili la Mdodo pilau.

4.2.39 Etimolojia ya Jina la Bumbwini

Bumwi ni aina ya chakula ambacho hupikwa kwa kutumia mchele au chenga za mchele, mchele huo hutangwa na baadae huchanganywa na nazi iliyokuwa

haijachujiwa huwekwa na sukari baadae huviringwa mithili ya badia, chakula hichi hutumika mashghulini.

Majina ya Mahali Yanayofanana na Wanyama au Wadudu

Halkadhalika kuna baadhi ya majina ya mahali yaliyopewa majina kutokana na wanyama Chum (1982) anaeleza asili ya mitaa inayopatikana Mkoa wa Kusini Unguja. Anatoa mfano wa *Paje,* kwamba asili yake ni mnyama aitwae paa nae mtafiti amegundua majina haya baada ya kufanya majadiliano ya pamoja, usaili na dodoso na amegundua kwamba yapo majina yanayofanana na wanyama, ambayo ni kama yafuatayo;

4.2.40 Etimolojia ya Jina la Mbuyu Popo

Popo ni ndege mashuhuri sana katika kisiwa cha Unguja, ambao hupatikana sana vijijini hii ni kutokana na kuwepo kwa miti mingi vijijini kuliko mjini kwani ndege hawa hupendelea kukaa juu ya miti na husikika sana wakati wa usiku, hivyo kijiji hichi kimeitwa Mbuyu Popo kwa sababu ya kuwepo popo wengi ambapo ilikuwa ikifika wakati wa usiku wanaenda kukaa juu ya Mbuyu huo, ni kijiji ambacho kipo katika Jimbo la Mkwajuni katika Shehia ya Matemwe.

4.2.41 Etimolojia ya Jina la Kiembe Samaki

Hili ni miongoni mwa mitaa maarufu huko wilaya ya Kaskazni A unguja, ambapo samaki ni miongoni mwa kitoweo ambacho kinapendwa sana Zanzibar, mtaa huu umefananishwa na samaki kwa sababu watu waliokuwa wanavua samaki pwani walikuwa wakishawapata samaki wanakwenda sehemu ambayo kuna muembe na

wanawaweka samaki wao kwa ajili ya kuwaua, na hii ndio sababu sehemu hiyo ikaitwa kiembe samaki, ni kutokana na kuwa kunawekwa samaki kwenye muembe.

4.2.42 Etimolojia ya Jina la Paaguu

Hili ni jina la mtaa ambalo limepewa jina hili kutokana na huyu mnyama anayeitwa paa, mtaa huu umeitwa hivyo kwa sababu katika sehemu hiyo kulikuwa na paa, alikuwa anakimbia hivyo watu walikuwa wanamfukuza kwa miguu na ndio maana pakapatikana jina la paaguu, ni mtaa uliopo katika shehia ya Matemwe katika jimbo la Nungwi.

Majina ya Mahali Yanayotokana na Watu Mashuhuri

Katika jamii kuna watu ambao wanajuulikana zaidi kutokana na mambo wanayoyafanya, hali hii hupelekea hata majina ya mitaa kupewa majina yao, Kwa mfano, Haji, (2001) katika kazi yake ya uchanganuzi wa kiisimu jamii wa mfumo wa utoaji wa majina ya mitaa alichunguza asili ya mtaa wa kwa Mwinyi mkuu na akagundua kuwa kuwa asili yake ni jina linalotokana na mwinyi mkuu aitwae Muhammad bin Ahmad na pia katika kazi hii mtafiti ameyagundua majina ya watu mashuhuri baada ya kupata taarifa kutoka kwa watafitiwa wake.

4.2.43 Etimolojia ya Jina la Khamisi Bweni

Huu ni mtaa uliopo Wilaya ya Kaskazini A, ambao ni mtaa ambao unatokana na watu Mashuhuri hii ni kwa sababu Bi Mwajabu amesema Khamisi Bweni ni mtu wa mwanzo ambaye amevumbua liko au diko ambao alikuwa anautumia kwa kuegesha mtumbwi wake kila anapokwenda baharini na kurudi, hivyo mpaka sasa wavuvi

wanatuma diko kwa ajili ya kuegesha mitumbwi yao na hii ndio sababu sehemu hiyo ikaitwa hivyo.

4.2.44 Etimolojia ya Jina la kwa Helefu

Jina hili la mtaa limepewa jina la mtu mashuhuri ktokana na umaarufu wa mtu huyu,kwani ni muarabu na ni mtu wa mwanzo kujenga horofa katika jimbo la Bumbwini, ni mtu ambaye shughuli zake ni kulima na kuvunja nazi,maelezo haya yalipatikana katika mahojiano ya hivyo kutokana na shughuli hizo ndizo zilizomfanya mtu huyu kuwa marufu na mwenye kujuulikana.

4.2.45 Etimolojia ya Mtaa wa Siti Mwinyi

Huu ni mtaa ambao upo katka jimbo la Donge, katika dodoso wengi walitoa asili ya jina hili kwamba jina hili la Siti Mwinyi limetokana na kuwa mtu huyu alikuwa ni mke wa Mzee Ali Hassan Mwinyi kipindi ambacho alipopata uraisi wa Zanzibari ambapo ilikuwa ni katika mwaka 1980 mpaka 1990 kutokana na umaarufu wa mtu huyu ikapelekea mpaka familia yake kuwa maarufu na ndio maana likapatikanajina hili la Siti Mwinyi japo kuwa yeye mwenyewe hayupo tena lakini jina bado lipo na linaendelea kudumu.

4.2.46 Etimolojia ya Mtaa wa Makame Ng'ombe

Huu ni mtaa ambao umepewa jina la mtu mashuhuri anayejuulikana sana na watu wengi, Umashuhuri huu unatokana na shuguli zake za ufugaji . Mtu huyu alikuwa ni mfugaji mzuri wa ng'ombe. Mtu huyu alikuwa na ng'ombe wengi ambao alikuwa anauza. Bwana huyu alikuwa akijulikana kwa umashuhuri wa Makame ng'ombe na

eneo aliloishi lkaitwa kwa Makame ng,ombe. Maelezo haya yanatokana na bwana mmoja aitwae mzee Ali ambae anaishi katika mtaa huu.Hivyo majina ya mahali yametubainishia kwamba hayakuja kiholelaholela bali kulikuwa na historia ambazo zimewafanya wanajamii kutoa majina kulingana na historia hizo.

4.3 Kujadili Jinsi majina ya Mahali ya Kaskazini Unguja Yanavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja

Ni ukweli usiopingika kwamba kila jamii ina utamaduni wake. Watafiti wengi wamefanya chunguzi ambazo zimeonesha tamaduni za jamii mbalimbali. kwa mfano Omary (1970) katika kazi yake ya kuchunguza majina ya watu katika jamii ya Chasu aligundua kuwa Watoto wanaozaliwa katika kipindi vita wa kiume huitwa “Senkondo”, na watoto wa kike huitwa “Nenkondo”.

Hii inafanyika ili kudumisha tamaduni zao. Pia Zubeir (2015) katika kazi ya kuchunguza asili ya majina ya mitaa kaskazini Pemba aligundua kuwa jina la Micheweni linatokana na uchawi yaani imani za kishirikina. Kwa muktadha huo Zubeir akasema jina hili linaakisi utamadunu ya watu wa Pemba. Hata mtafiti wa kazi hii amegundua kuwa katika jamii ya Unguja kuna majina ya mahali yanayoakisi utamaduni wao. Ameyachambua majina hayo kama ifuatavyo:

4.3.1 Mtaa wa Batini unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja

Batini ni mtaa ambao unaakisi moja kwa moja utamaduni wa watu wa Unguja. Afisa wa utamaduni mkoa wa Kaskazini Unguja amesema kwamba jina la Batini limepatikana kwa kuwepo kwa sherehe za maulidi na ziara za madrasa. Sherehe hizi hufanyika kila mwaka. Kulikuwa na mabati maalumu ambayo yalikuwa yanatumika

kwa ajili ya kutiliwa wali, ambapo sherehe hizi vado zinaendelea kufanyika. Huu ni mtaa ambao upo katika jimbo la Bumbwini shehia ya Makoba.’’

4.3.2 Mtaa wa Mdodo Pungwa’ Unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja

Mtafiti alimuhoji mmoja kati ya wafanya kazi wa utamaduni kuhusiana na jina hili. Mfanya kazi huyo alisema kwamba, hii ni sehemu ambayo watu huwa wanacheza ngoma ya kiganga au ya kijadi ambayo inaitwa pungwa. Ngoma hii huchezwa kila ifikapo mfunguo nne kila mwaka. Sababu ya kupigwa na kuchezwa ngoma hii inadaiwa ni kutoa pepo anayeingia kwenye kichwa cha mtu.Ngoma hii huchezwaa kwa kuzunguka duara na baadae watu walio na pepo huchagawa. Sababu ya kuitwa pungwa ni kutokana na mtu ambaye alitoweka katika mazingira ya kutatanisha kwa muda mrefu. Baada ya muda kupita mtu yule akaja akatokea katika hali ya mazingara zingara. Watu walipomuona walifuatisha ule mdomo wake ambapo alikuwa akitamka hili neno la pungwa. Kuanzia hapo ndipo wakapiga ngoma na kuipa jina la pungwa. Huu ni mtaa ambao upo katika jimbo la Bumbwini. Huu ni mtaa ambao umepakana na vitongoji kama vile Jongoe, Mbuyuni na Mabandani.

4.3.3 Mtaa wa Muwange Unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja

Mama mmoja ajulikanae kwa jina la Bi Halima pamoja na mtumishi mmoja wa idara ya utamaduni wamekubaliana kuwa jina la Muwange lina akisi utamaduni wa jamii ya watu wa eneo hili. Jina la mtaa huu linalitokana na imani za kishirikina likiwa na maana ya kuwanga yaani kupiga ramli. Jina hii linaonesha dhahiri kuwa watu wa mtaa huu wana tamaduni za kishirikina ni mtaa unaosifikana kwa mambo ya kijadi hadi leo. Watu wengi wa mtaa huo wanaamini kwamba vikwazo na matatizo mengi yanayotokea katika maisha yao yanasuluhushwa kwa mambo ya kishirikina.

4.3.4 Mtaa wa Mwembe Mgaa na Utamaduni wa Watu wa Unguja

Mwembe Mgaa ni sehemu ambayo wanajamii wanaoishi Kaskazini Unguja hujumuika kwa pamoja baada ya mfunguo mtukufu wa Ramadhani. Mjumuiko wao unakuwa na shabaha ya kushereheka. Mgaa ni jina la ngoma ambayo watu huimba na kucheza kila ifikapo kipindi cha skukuu.

Wazazi huwapeleka watoto wao kwa ajili ya kuwafurahisha ambapo hadi leo sehemu hiyo inatumika kwa ajili ya sherehe ya sikukuu. Kwa hivyo ni utamaduni wa jamii mzima ya Wazanzibari kufurahia kila ifikapo sikukuu na kuchagua maeneo maalumu ya kwenda kujifurahisha. Haya ni maelezo ya afisa utamaduni wa Kaskazini Unguja aliyoyata siku ya tarehe 2-6-2017 alipokuwa akihojiana na mtafiti wa kazi hii.

4.3.5 Mtaa wa Mdodo Pilau Unavyoakisi Utamaduni wa Watu wa Unguja

Kwa kawida chakula cha pilau ni chakula mashuhuri sana kwa Wazanzibari. chakula hiki hupikwa zaidi kwa ajili ya kuwakirimu wageni au ifikapo kipindi cha skukuu. halkadhalika chakula hiki hupikwa mashughulini kama vile harusini, msibani, maulidini kwenye ziara na shughuli nyengine za kijadi kama vile jando na unyago.

Mtafiti alipohoji kuhusiana na jina la Mdodopilau watafitiwa wengi walitoa hoja kwamba mahali hapa pameitwa Mdodo pilau kwa sababu ni sehemu ambayo palikuwa na muwembe mkubwa wa aina ya mdodo. Chini ya mti huo palikuwa ni kituo maalum cha kupikia pilau. Wanajamii wengi waliokuwa wakiishi eneo hili na pembezoni mwake walikuwa wakitumia eneo hili kupika. Bado utamaduni huo unatumika katika eneo hilo.

4.5.6 Kijiji cha Kivunge na Utamaduni wa Watu wa Unguja.

Kivunge ni mtaa ambao upo katika wilaya ya Kaskazini A. Mtaa huu upo katika barabara inayoelekea Nungwi. Huu ni mtaa ambao watu wengi wanaufahamu kutokana na kuwa upo maeneo ya ya soko na stendi ndogo ya magari ya kuelekea Mkokotoni kwa upande mmoja na Nungwi kwa upande wa pili. Mtaa huu unaakisi utamaduni wa watu wa eneo hili kutokana na kuwa umepewa jina hili la kivunge kwa sababu watu wa hapo walikuwa na utamaduni wa kuvunga vunga mambo yao katika Nyanja mbalimbali za kimaisha. Hawakuwa wazi katika shughuli zao kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Watu hawa walikuwa hawapendi mambo yao yajuuikane na watu wengine. Hata hivyo watu hao walikuwa wanaishi kwa umoja na mashirikiano katika mambo yao.

4.3.7 Mtaa wa Dunduwa na Utamaduni wa Watu wa Unguja

Dunduwa ni jina la mtaa ambao upo katika Jimbo la Bumbwini Wilaya ya Kaskazini B., ambapo vijana watano katika dodoso zao wamesema kuwa ni jina hilo linaloakisi moja kwa moja utamaduni wa jamii husika. Asili ya jina lake ni kwamba kulikuwa na dundu ambalo lilikuwa ni kifaa mithili ya firimbi fulani. Kifaa hicho kiliokotwa kutoka pwani. Kifaa hicho kilipokuwa kikipulizwa watu wa sehemu hiyo hujumuika kwa pamoja kwa ajili ya kucheza na kuimba., Ngoma waliokuwa wakicheza ilikuwa inaitwa dunduwa kutokana na hilo dundu lililokuwa linapulizwa. Hii inaonesha wazi kwamba watu wa eneo hili wana utamaduni ya kucheza ngoma ya dunduwa.

4.3.8 Mtaa wa Muwele na Utamaduni wa Watu wa Unguja

Muwele ni mtaa ambao upo katika jimbo la Donge. Katika majadiliano ya pamoja yaliyofanyika siku ya tarehe 6/7/2017-wahojiwa wamekubaliana kuwa huu ni mtaa

ambao jina lake lina uhusiano wa moja kwa moja na utamaduni wa jamii husika. Hii ni kwa sababu Muwale lina maana ya mwari ambaye anatibiwa na mganga.Watu wa mtaa huu walikuwa na utamaduni wa kuwapeleka wari wao kwa waganga kwa ajili ya kutibiwa. Matibabu hayo yalihusu matatiizo mbali mbali kama vile matatizo ya Kiswahili, matatizo ya kutopata waume na mengineyo. Hadi leo bado utamaduni huo wa kuwapeleka wari kwa waganga upo.

4.4 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza asili za majina ya mahali ya Kaskazini Unguja jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja, matokeo ya utafiti huu yameongozwa na malengo mahsusi mawili ambayo ni kuchunguza asili za majina ya mahali ya Kaskazini Unguja na Kufafanua majina ya mahali ya Kaskazini Unguja jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja.

Katika lengo la kwanza ambalo ni Kueleza majina ya mahali ya Kaskazini Unguja, matokeo ya Utafiti huu yameonesha wazi kwamba lengo hili limefikiwa kwa kiasi kikubwa kwani mtafiti amepata taarifa kutoka kwa watafitiwa wake ambazo ni za ukweli na uhakika kwani mtafiti amegundua kwamba majina ya mahali hayajaja tu kiunasibu kwani kuna matukio ambayo yamesababisha kutokea kwa majina hayo, asili ya majina hayo yanaonesha wazi kwamba yanaitambulisha jamii hiyo kwani ni majina ya kipekee ambapo jamii nyengine hayana majina kama hayo kama alivyosema Afisa Utamaduni wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwamba *majina ya mahali chanzo chake ni wanajamii wenyewe, baadae jina hilo huwasilishwa wilayani kwa ajili ya kupata usajili na kujuulikana kitaifa, aliendelea kusema kwamba hakuna taasisi iliyowekwa*

ya kushughulikia majina ya mtaa katika wilaya hadi Mkoa bali hutumiwa na watumiaji kutokana na sababu zao wenyewe, hivyo ni wazi kwamba majina ya mahali ni utambulisho wa jamii husika.

Katika lengo la pili ambalo ni kujadili asili za majina ya mahali ya Kaskazini Unguja jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja, halkadhalika lengo hili limefikiwa kwani mtafiti amegundua kwamba kuna baadhi ya majina yana uhusiano wa moja kwa moja kati ya jina husika na utamaduni unaofanyika katika eneo hilo, na hii ni kutokana na kutambulisha mila na desturi zinazofanyika katika jamii hiyo, hivyo taarifa za watafitiwa zimemuwezesha mtafiti kufanikisha utafiti huu.

4.5 Hitimisho

Sura hii imechanganua na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojiano na usaili Uwasilishaji wa uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo maalumu ya utafiti. Na umeongozwa na mkabala wa maelezo na kiidadi. Aidha, nadharia jumuishi ya Gilles imeongoza katika kuchanganuwa data. Utafiti huu umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani umekidhi malengo ya utafiti huu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi wa Sura ya Tano

Baada ya utafiti kukamilika, katika sura hii inahusu juu ya muhtasari wa utafiti mzima, pamoja na matokeo ya utafiti na jinsi nadharia iliyotumika ilivyofikiwa, hitimisho juu ya utafiti husika pamoja na mapendekezo.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulihusu etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Unguja jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja, utafiti huu ulifanyika katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ukijumuisha wilaya ya Kaskazini A na wilaya ya Kaskazini B, ambapo mtafiti ameteua majimbo sita na baadhi ya shehia zake, majimbo ambayo mtafiti ameyateua ni Nungwi, Tumbatu, Mkwajuni, Chaani, Donge na Bumbwini katika mchakato mzima wa utafiti, mtafiti aliwajumuisha watafitiwa mbalimbali wakiwemo wafanya kazi wa mambo ya kiutamaduni, wazee na vijana. Mtafiti alizikusanya taarifa zao kwa mbinu ya dodoso, hojaji pamoja na majadiliano ya pamoja kwa kuongozwa na malengo na maswali ya utafiti.

Mtafiti amekusanya taarifa za watafitiiwa wake kwa kuongozwa na malego mahsusi mawili ambayo ni kueleza asili ya majina ya mahali ya Kaskaazini Unguja, katika lengo hili mtafiti aligundua kwamba majina ya mahali yana asili ambazo zinatokana na historia ya matukio yaliyotokea hapo kale, au vitu vya asili ambavyo vinawakilisha majina hayo, miongoni mwa vitu hivyo bado vipo lakini vyengine vimebadilishwa kwa mfano Batini mtaa huu umeitwa hivi kutokana na kuwepo kwa mabati ya

kupakulia wali wakati wa harusi lakini kwa sasa zinatumika sahani badala ya mabati. Halkadhalika katika lengo hili mtfiti aligundua kuna majina ya mahali yanayofonana na miti, wanyama vyakula na hata watu mashuhuri.

Kujadili jinsi majina ya mahali ya kaskazini Unguja yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja, hapa mtafiti aligudua kwamba kuna baadhii ya majina yanaakisi moja kwa moja ule utamaduni uliokuwepo, au uliopo katika sehemu husika. Majina hayo ni Mdodo Pungwa, ni utamaduni wa ngoma ya kichawi ambayo kila mfunguo nne inachezwa. Mdodo Pilau ni kutokana na chakula mashuhuhuri kinachopikwa mashughulini. Muwange ni utamaduni wa imani za kishirikina. Kivunge ni utamaduni wa kuvungavunga mambo ya kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa,.Muwale linatokana na wari wanaofanyiwa dawa za kiganga. Muwembe Mgaa ni utamaduni wa kuwepo kwa sherehe katika sehemu hiyo kila baada ya mwezi mtukufu wa ramadhani, na Dunduwa ni kuwepo kwa firimbi ambayo inaashiria watu kukusanyika kwa pamoja na kucheza ngoma.

Kwa upande wa nadharia tuliyoitumia ambayo ni nadharia jumuishi ya Gilles matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba nadharia hii imekidhi malengo ya utafiti huu kwani imeonesha kuwa wanajamii husika ndio wanaoyapa majina ya mahali katika maeneo wanayoishi, hii ni kutokana na kuwepo kwa mshikamano baina ya wanajamii hao, hivyo wanajamii hao imebainika kuwa majina haya hutolewa kulingana na matokeo yaliyokuwepo enzi za zamani, halkadhalika utoaji huo wa majina huzingatia kwa kuwepo miti, wanyama, vyakula na hata watu mashuhuri.

Ukubalifu wa majina hayo unatokana na wanajamii husika kwani matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba wanajamii wameyakubali majina hayo ili yatuumike kwa

ajili ya kuitambulisha jamii yao, halkadhalika kuutambulisha utamaduni wao, Tajel (1982) *anasema kuwa Utambulisho ni namna mtu anavyojichukulia yeye mwenyewe kuwa ni mwanajamii wa jamii fulani pamoja na thamani na umuhimu wa kuipa jamii hiyo kwa kuona kuwa ina umuhimu wake*, hivyo ni dhahiri kwamba utambulisho ni jambo muhimu katika jamii yoyote ile, na si majina ya mahali pekee yanayoitambulishha jamii tu bali kuna mambo mengine mengi yanayoitambulisha jamii kama vile majina ya watu, majina ya familia, muonekano wa mtu husika, mila na desturi, lugha na mengineyo.

5.3 Hitimisho la Utafiti

Utafiti huu umetupa mwanga ya kuwa majina ya mahali hayatokei tu kiholela holela bali kuna mambo ambayo yamepelekea kutokea kwa majina hayo, hivyo katika utafiti huu tumebaini kuwa majina ya mahali yana uhusiano mkubwa wa jamii husika, halkadhalika tumeona jinsi ambavyo wanajamii hutoa majina kwa kutumia vigezo mbali mbali kama vile kuwepo kwa miti, wanyama vyakula na watu mashuhuri. Kwa ujumla tunaema kwamba asili za majina ya mahali ya Kaskazini unguja yanatokana na watu wa Unguja na kuna mengine yanatkana na wahamiaji waliotoka sehemu mbali mbali na kuhamia Unguja kutokana na shughuli mbali mbali kama vile uvuvi, kilimo, ufugaji na kadhalika.

5.3 Mapendekezo ya Jumla

kwa kuwa lengo kuu la utafiti ni utafiti huu ni kuchunguza asili za majina ya mahali ya Kaskazini Unguja jinsi yanavyoakisi utamaduni wa watu wa Unguja hivyo kutokana na lengo hili mtafti mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo;

Majina yoyote yale yanayotumika katika jamii fulani ambayo yanawatambulisha wanajamii hao ni vyema yakawa yanajuulikana na vizazi vipya na vikongwe, hiyo mtafiti anaipendekeza serekali kuwaajiri watu maalumu kwa ajili ya kuyaweka katika kumbukumbu kwa kuyaandika au hata kuyarikodi vizazi vinavyokuja viweze kuyafahamu kwa kina majina hayo. Vile vile mtafiti anapenda kutoa mapendekezo kwa wanajamii kuyaenzi na kuyatunza majina ya maeneno wanayoishi kwa sababu ni miongoni mwa mambo ambayo yanaitambulisha jamii hiyo.

5.4 Mapendekezo ya Tafiti za Baadae

Utafiti huu sio kikomo cha cha kutafiti eneo la Kaskazini Unguja, hivyo ni vizuri zaidi kwa watafiti wa baadae kutafiti vipengele na mambo mengi yanayohusu watu wa jamii hiyo kama vile msamiati wa lugha, majina ya watu, na hata majina ya mahali kwani kuna vijiji vingi ambavyo vinahitajika kufanyiwa kazi, na pia kuna baadhi ya majina ya kaskazini Unguja yanabadilika kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia nalo hili pia linahitajika kufanyiwa kazi.

MAREJELEO

BAKIZA, (2008). *Utamaduni wa Mzanzibar*, Zanzibar: BAKIZA.

Baver, H. D. R., (1979). *Chinese Family and Kinship.* New York: Colombia University Press.

Best, J. W., na Kahn, J. V. (1993). *Research in Education.* Washington DC: Allyn and Bacon.

Boas, F., (1964), *"On Geographical Names of the Kwakiuti Indians"Language in Culture and Society, A Reader in Linguistics and Anthropology*. New York: Berkeley Harper and Row Publishers.

Cameroon, K. (1961). *English Place Names*. London: Exford University Press.

Chulk, O. O. (1992). *Names fromAfrica: Their Origin, Meaning and Pronoucition,* Chicago: John Publishing co Cooper.

Chum, H. (1982). *Desturi na Mila Zetu*. Arusha: East Africa Publication Limited.

Enon, D. C. (1998). *Educational Research, Statistics and Measurements,* Uganda: Department of distance Education, Makerere University

Funk, E. R. (1997). "*The Power of Naming*" Imepatikana tarehe 21/3/2017 katika http://feministe com/archives/v/4/malefen.html.

Habwe, J., na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Haji, M. M. (2014). Uchanganuzi wa Kiisimujamii wa Mifumo ya Utoaji Majina ya Mitaa katika Mkoa wa Kusini Unguja: (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Uganda, Kampala, Uganda.

Joho, H. A. (2011). Matumizi ya Majina katika Utambulisho wa Jamii ya Watanzania: (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.

Khamis, A. M., na Madumula, J. S. (1989). *"Majina Yanayohusu Watu"* Mulika o.21, Dar es Salaam TUKI.

Kofi, A. (2006). "The Sociolinguistic of Akan Personal name", *In Nordric Journal of African Studies, 15(2),* 206-235.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Afrika.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology.Method and Techniques, Second Edition*, New Delhi: New Age International (P) ltd.

Manyasa, J. (2008). Investigating the Basis of Naming People in Kisukuma, Unpublished M.A. Dessertation, University of Dar es Salaam, Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2004). *Sarufi Maumbo Ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam : Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massoud, A. M. (2014). Mchango wa Majina na Vijiji vya Donge katika Kuhifadhi Historia ya Unguja Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro: Tanzania.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha*. Mwanza : Serengeti Educational Pubisher Ltd.

Mgullu, R. S. (2002). *Mtalaa wa Isimu, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.

Mlacha, S. A., na Hurskainen, A. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu Jamii, Sekondari na Vyuo*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mutembei, A. K. (2009). *UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili*. Chou Kikuu Dar es Salaam, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Muzale, H. R. T., (1996). Linguistic and Social-Culture Aspects in Interlacanstrine Bantu Names" *Kiswahil, 61(2),* 28-49.

Mzee, S. Y. (2004). *Nafasi ya Majina ya Mzimu wa Pepo katika Pepo za Makunduchi katika Kuhifadhi Utamaduni wa Makunduchi.* Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro (Haijachapishwa), Dar es Salaam, Tanzania.

Omary, C., and Richerds, I. A. (1966). "Person Names in Social-Cultural Context" Jarida la Kiswahili la Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili. *Journal of the Institute of Swahili Research, 40(2),* 52 – 71.

Pandu, R. S. (2014). Asili ya Majina ya Shule za Unguja Mjini katika Kutunza Historia ya Zanzibar. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro, Tanzania.

Redio Nour, (18/10/2013). *Kipindi cha Tutunze Historia Yetu Redio Zanzibar*: Nour.

Schotsman, P. (2003). *A Grammar of Runyambo Language of Tanzania* (LOT) Project Universityu of Dar es Salaam. LOT Publisher.

Seif, D. G., (2011). *Nyimbo za Jando katika Jamii ya Kikaguru, Kata ya Gairo,* Tasnifu M.A. Kiswahili.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinch*i. Dar es Salaam: Al-amin Education and Research.

TUKI, (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University.

VIAMBATANISHO

Kiambatisho i: Maswali ya Dodoso kwa Vijana wa Mkoa wa Kaskazini Unguja

MADA: ETIMOLOJIA YA MAJINA YA MAHALI YA KASKAZINI UNGUJA NA JINSI YANAVYOAKISI UTAMADUNI WA WATU WA UNGUJA

SEHEMU A: MAELEZO KUHUSU MADA HUSIKA

Tafadhali ndugu mwananchi unaombwa ushirikiano kwa kujibu maswali hayo hapo chini yenye lengo la kufanikisha zoezi hili la utafiti na wala si vyenginevyo, jibu kwa kuweka alama ya vyema katika kisanduku cha jibu ulilolichagua, na toa maelezo kwa kadri swali linavyokutaka ufanye.

1. Mtaa unaoishi unaitwaje?.....

2. Taja mitaa mingine mitano ambayo ipo karibu na sehemu unayoishi.

i).....ii).....iii).....

iv).....

3. Tunafahamu kwamba hakuna jina hata moja lililozuka bila ya kuwa na sababu zake za msingi, hebu tutajie majina ya mitaa angalau mitatu ya kaskazini Unguja huku ukieleza kwa nini jina hilo limezuka?

i)Mtaa.....

a)Umeanza lini.?.....

b)asili yake ni ipi?.....

c) mipaka yake ni ipi?.....

i).....

.....

ii).....

.....

4. Katika majina yafuatayo yana historia ya kuonesha utamaduni wa Wazanzibari, Eleza historia hizo japo kwa ufupi

Nungwi.....

.....

Bumbwini.....

Mkwajuni.....

.....

Tumbatu……

……

Muwange

……

5. Kuna majina ya mitaa ya kaskazini Unguja ambayo yamepewa majina yanayofanana na vyakula, kama yapo nitajie miwili na kwa nini yameitwa hivyo

.....

.....

6. Taja mitaa mitatu ya kaskazini Unguja yenye majina ya wanyama, na toa maelezo kwa nini ikaitwa majina hayo

.....

.....

7. Taja mitaa ya kaskazini Unguja ambayo majina hayo yamefanana na majina ya mimea au miti na eleza kwa ufupi kwa nini yameitwa hivyo

……

……

……

8. Taja mitaa miwili ya kaskazini Unguja yaliyopewa majina kulingana na watu mashuhuri, na toa maelezo kwa nini yameitwa hivyo

……

……

9. Jee majina ya mitaa ya kaskazini Unguja yanaakisi utamaduni wa Unguja, kama jibu lako ni ndio eleza kwa ufupi jinsi yanavyoakisi

……

10. Una maoni gani kuhusiana na kudumisha na kuendeleza utamaduni wa Wazanzibari ……

AHSANTE SANA KWA MASHIRIKIANO YAKO

Kiambatisho ii: Maswali ya Hojaji kwa Wazee na Wafanyakazi wa Mambo ya Kiutamaduni

MADA: ETIMOLOJIA YA MAJINA YA MAHALI YA KASKAZINI UNGUJA NA JINSI YANAVYOAKISI UTAMADUNI WA WATU WA UNGUJA

MAELEZO

Hojaji hii ina lengo la kukusanya taarifa kuhusiana na mada husika, maswali yatajikita katika majina ya mahali, historia yake, asili yake na utamaduni wake, Tafadhali jibu maswali yote kwa kutoa taarifa kwa mujibu wa uelewa wako.

MASWALI

1 Ni ipi historia ya mtaa unaoishi

2 Kwa kawaida mitaa mingi hupewa majina kutokana na historia fulani tutajie shehia zozote za Kaskazini Unguja unazozifahamu pamoja na historia zake

3 Mitaa gani ambayo unafikiri inaonesha utamaduni wa watu wa Unguja na eleza ni utamaduni gani huo

4 Taja mitaa ambayo haioneshi utamaduni wowote ule wa watu wa Unguja

5 Jee kuna uhusiano gani kati ya majina ya mitaa na utamaduni

6 Kutoka na mabadiliko ya kila siku, jee majina ya Kaskazini Unguja yanabadilika, Toa sababu

7 Kwa maoni yako unafikiri kuna athari yoyote inayopatikana kutokana na utoaji wa majina ya mahali

8 Tuelezee faida na hasara za kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wa watu wa Unguja

9 Kwa vile umeishi muda mrefu unawafahamu watu wengi mashuhuri hebu tutajie majina ya mitaa ya kaskazini Unguja ambayo yamepewa majina kulingana na watu mashuhuri

ASANTE SANA

Kiambatisho iii: Maswali ya Majadiliano Kati ya Wazee na Vijana

1 Ni ipi historia ya mtaa huu?

2 Hebu tujadili asili za mitaa yoyote mitano (5) iliyopo katika jimbo la Nungwi na Donge

3 Kuna baaadhi ya majina ya mitaa yanaakisi moja kwa moja utamaduni wa Watu wa Unguja, Taja majina hayo na jadili kwa jinsi gani yanaakisi utamaduni huo?

4 Majina ya mahali yapo yaliyofanana na mimea, wanyama, vyakula, watu Mashuhuri na hata wanyama, hebu tujadili majina hayo

5 Katika jimbo la Bumbwini, Tumbatu, na Mkwajuni, majimbo yote haya yana shehia zake tutaje na tueleze asili za majina ya shehia hizo

6 Kuna majina ya Kaskazini Unguja ambayo yamepata athari yoyote, kama yapo yataje na eleza athari hiyo

7 Ni kwavipi tunaweza kuyalinda na kuyahifadhi majina ya mitaa yetu

ASANTENI KWA MASHIRIKIANO YENU